## JONGEENI WABARIKIWA WA BABANGU.Zab. 1.

Kiitikio: Jongeeni wabarikiwa wa babangu,jongeeni ingieni nyumbani pa Bwana.

1. Heri mtu asiengia barazani mwa mkosefu/wala asiyesimama njiani pa mpotevu.
2. Heri mtu asiyekaa kitini pa wachekaji/Bali apendaye sheria ya Yahwe na kuinonona kutwa kucha.
3. Yu sawa mti kupandwa karibu na mto/Kutoa matunda pa wakati unaofaa.
4. Majani yake hayakauki kamwe baraka ninaye/mfano mwema kwa wakosefu,mfano mwema.
5. Hao kweli ni sawa makapi yaliopeperushwa hewani/Kweli wakati wa maamzi waovu watashindwa.
6. Watashindwa wakosefu barazani mwa mwenyi haki/na njia zao hazitatambulika.
7. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho/Kama mwanzo na daima na milele Amen.

## ANASA ZA DUNIA ZINAPEPERUSHWA: Zab. 2.

Kiitikio:Anasa za dunia zinapeperushwa sawa mavumbi,heri anayeshika sheria ya Bwana.

1. Mbona makabila hutoa kelele/hunguruma vilio vya bure,wafalme wa Dunia wanasimama,waserkali huwasha fitina kwa Yahwe na mpakwae.
2. Haya tuvunje vyao vizuio/tupasue yao nira/Anayetawala mbinguni huwachekea/Huwachekea kweli Yahwe mfalme.
3. Hapo katika hasira yake huwanenea/kwa hasira yake wapigiwa woga kali/Ndimi niliempaka wangu mfalme/Juu ya Sioni mlimangu mtakatifu.

4. Yahwe ameniambia u mwanangu/Ndimi niliyekuzaa leo/
Uombe nikupe makabila yawe urizi wako/Utawale hata miisho ya Dunia.
5. Utawavunja kwa mti wa chuma/vipande vipande sawa vyombo vya udongo.
6. Ndipo hapo wafalme sikieni/Jifunzeni waamzi wa Dunia/Mtumikieni Yahwe kwa uchaji/Migue muibusu kwa kutetemeka.
7. Angekasirika mungeangamia/Kumbe kwa rafla hasira yake huwaka/
Atukuzwe Baba na Mwana na Roho/kama mwanzo na daima na milele Amen.

YAHWE USIMAME UNIOKOE Zaburi 3.

Kiitikio: Haya,Yahwe,haya Yahwe usimame usimame,uniokoe,ewe Bwanangu,Ee Yahwe Yahwe.

1. Ee Yahwe wachokozi wangu ni wengi/ wengi tena wasiopatana nami.
2. Wengi huonea moyo wangu wakisema/katika Mungu hakuna wokovu kwako.
3. Lakini,ee Bwana u ngao yangu/ u sifa yangu unasimika kichwa changu.
4. Napaliza sauti nalia kwa Yahwe/tokea mlimae mtakatifu ananijibu.
5. Nami najilaza nashikwa na usingizi/Yahwe anitegemea ninapoamka.
6. Siogopi watu hao wajapo mamia/ Kunichungulia najicho baya pahali pengi.
7. Ee Yahwe wapiga shavuni washambulizi wangu/wavunja meno ya wawatu waovu.
8. Wokovu hutoka katika Yahwe/Taifa lake hupewa Baraka.
9. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho/kama mwanzo na daima na milele Amen.

## KARIBUNI ENYI MWAKOSAO NGUVU Zab.4

Kiitikio: Karibuni enyi mwakosao nguvu,nami ntawapa chakula kitakacho walisha kwa heri ya milele.

1. Ee Mungu wa haki uniitikie nikuombapo/uondoe kwa huruma shida zangu za roho.
2. Enyi wanadamu hata lini mutafungwa moyo/Mwarizikia upuuzi mwasifu uongo.
3. Mwamini wa Bwana hutendewa maajabu/nasikilizwa ni mwitapo.
4. Mjute moyoni simchukieni Bwana/Hata kitandani fikirini salama.
5. Mtolee sadaka Rabi mkarimu/Msikose kitumaini kwa mkubwa wenu.
6. Wengi husema nani atatuonyesha raha/Bwana utuinulie nuru ya uso wako.
7. Unilinde Bwana njiani mwa haki/Ufukuze mbali wanaotaka kunidanganya.
8. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho/Kama mwanzo na daima na milele Amen.

## WANAOKAA KWAKO WAJALIWA HERI. Zaburi 5

Kiitikio: Wanaokaa kwako wajaliwa heri,furaha inadumu milele kwao.

1. Bwana uyasikilize maneno yangu/Malalamiko yangu uyatambue.
2. Uwe msikilivu ninapokuita/ ewe mfalme wangu na Mungu wangu.
3. Kwako naelekea maombi yangu ee Bwana/ Sauti yangu unaisikiliza asubui.
4. Asubui nakuwekea makusudi yangu/Halafu nakesha vema.
5. Ndiwe Mungu hupatani na uovu/ Mtu mbaya hapewi kiti kwako.
6. Nami kwa wingi wa mapendo yako/ Nakubaliwa nyumbani kwako.
7. Mwamini abarikiwa nawe Bwana/Sawa ngao neema yako inamkinga.
8. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho/ Kama mwanzo na daima na milele Amen.

## UYAPOKEE VEMA MAOMBI YANGU. Zaburi 6.

Kiitikio: Nakusihi, ee Bwana nakusihi;uyapokee vema maombi yangu.

1. Usiniazibu Bwana katika yako asira/Usinijibie unapokasirika.
2. Uniwie razi Bwana nakosa nguvu/Unigange mifupa yangu imegeuka.
3. Moyoni mwangu uzaifu ni mwingi/Hata lini Bwana utakaa mbali nami.
4. Unirudie Bwana uponye moyo wangu/uniokoe kwa ajili ya mapendo yako.
5. Kwani,kaburini hakuna anayekukumbuka/kuzimuni nani atakayekusifu.
6. Watenda uovu waniepukie mbali/Kwani Bwana asikia malalamiko yangu.
7. Bwana asikia kusihi kwangu/Bwana atapokea vema maombi yangu.
8. Maadui yangu washindwe,wapigiwe haya/Warudi nyuma wapigiwe haya kwa rafla.
9. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho/Kama mwanzo na daima na milele Amen.

## EE YAHWE JINA LAKO KUBWA SANA. Zaburi 8.

Kiitikio: Ee Yahwe Bwana wetu,ee Yahwe,jina lako tamu na kubwa sana,ulimwinguni litangazwe na liheshimiwe kote.

1. Utukufu wako ni juu ya ulimwengu/midomo ya watoto wadogo yapenda kuimba.
2. Unasimika nguvu zako kwa mshambulizi/kusudi uwashinde maadui na wakaidi.
3. Tukitazama mbingu kazi ya mkono wako/mwezi na nyota ulizotiako.
4. Mtu anakiasi gani hata umkumbuke/Mwanadamu hata umwangalie.
5. Ulimwumba karibu sawa na Mungu/Ukimvika taji la ukuu na la sifa.

6. Ulimpatia utawala juu ya kazi ya mikono yako/uliweka vitu vyote chini ya miguu yake.
7. Ee Yahwe Bwana wetu/Jina lako kubwa sana duniani popote.
8. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho/Kama mwanzo na daima na milele Amen.

## KIVULINI MWAKE BWANA Zaburi 16.

Kiitikio: Njia ya wapotevu sitaifuata kamwe/Haya nitatembea kivulini mwake Bwana.

1. Usikilize Bwana haki yangu/Usigeuke uso ninapokuita.
2. Usikilize ninapokuomba/Midomoni mwangu hakuna hila.
3. Hukumu yangu itatoka usoni mwako/Macho yangu yakubalia mambo ya haki.
4. Kwa wale wasimamao kuumeni kwako/Unikinge sawa mboni ya jicho.
5. Unifiche kivulini mwa mabawa yako/Waovu wasipate kunishambulia.
6. Maadui huwaka tamaa kunizungukia/ Sawa simba tayari kurarua.
7. Usimame Bwana uende kuwaangusha/ Uondoe roho yangu mkononi mwa mpotevu.
8. Atukuzwe Baba ,na Mwana, na Roho/ Kama mwanzo na daima na milele Amen.

## BWANA YU MCHUNGA WANGU. Zaburi 22.

Kiitikio: Bwana yu mchunga wa roho yangu,sikosi neema zake hasha.

1. Bwana yu mchunga wangu;sikosi kitu hasha;kwenyi malisho mabichi ndipo aliponilaza.
2. Kwenyi maji,ya kuburudisha,ndipo atanipumzisha,roho yangu ameishibisha.
3. Ameniongoza,katika njia ya haki,kwa ajili ya jina lake.
4. Hata ninapoingia,katika bonde la mauti,sitaogopa maovu,kwa kuwa wewe u nami.

5. Uchungaji na maongozi yako,hayo yanituliza.
6. Meza,umeniandalia,mbele ya wachokozi wangu.
7. Kichwa umenipaka mafuta,kikombe changu kimefurika.
8. Rehema na neema zanifuata,siku zote za maisha yangu.
9. Nyumbani mwa Bwana nikae,hata nyakati zilizo mbali.
10. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho,kama mwanzo na daima na milele Amen.

VYOTE MALI YA MWENYEZI Zaburi 23.

Kiitikio: Ashangiliwe,huyu mfalme,anayekuja kwa jina la Bwana Ashangiliwe.

1. Kwake Bwana ulimwengu,na vyote vilivyomo,dunia na wote wakaako.
2. Nani atakwea,mlimae Mungu milele,nani atafikia pahali patakatifu.
3. Aliye na mikono minyofu,na moyo mwadilifu,asiyehapa kwa udanganyifu.
4. Yule atapewa,baraka ya juu,na wokovu wa Bwana mkarimu.
5. Ndio urisi,wa taifa limwombalo,na watu wamwelekeao Mungu wa Yakobo.
6. Panueni milango ,inueni visingiti,mfalme wa sifa akaribia.
7. Mfalme huyu nani,ndiye Bwana mwenyezi na nguvu bora,Bwana wa majeshi mfalme wa sifa.
8. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho,kama mwanzo na daima na milele Amen.

## KARAMUNI MWA BWANA. Zaburi 30.

Kiitikio: Karamuni mwa Bwana nyoyo zetu hushiba,hulishiwa uzima wa milele.

1. Fazili zako ni nyingi Bwana/Kwa ajili ya wote wakuchao.
2. Wakukimbiliao wapata tulizo/Mbele ya macho ya wanadamu.
3. Unawakinga kwa mkono wa nguvu/wanaosumbuka kwa magumu.
4. Bwana atukuzwe yeye mkinga wangu/ Amenitendea fazili za ajabu.
5. Nami nalisema kwa haraka yangu/Kwani nimetupwa mbali ya macho yako.
6. Lakini ulisikia sauti ya maombi yangu/Palepale nilipokulilia.
7. Mpendeni Bwana enyi wanadamu/Enyi wateule wa taifa lake.
8. Bwana yu mkarimu kwa waaminifu wake/Bali huwalipia kwa ziada wenyi kiburi.
9. Simameni hodari inueni moyo/Chama kiteule munaomwendea Bwana.
10. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho/ Kama mwanzo na daima na milele Amen.

## ABARIKIWE YAHWE Zaburi 33.

Kiitikio: Abarikiwe Yahwe,asifiwe duniani kote,atujua,atupenda, atulinda,atukinga,anatufazilia.

1. Wakati wote nitambariki Yahwe/Sifa yake nitaisimulia daima.
2. Nafsi yangu inajisifu katika Yahwe/Wanyenyekevu wasikilize wafurahi.
3. Pamoja nami msifuni Yahwe/Pamoja nami mtukuzeni jina lake.
4. Namtafuta Yahwe ananijibu/Nakuondoa woga zangu zote.
5. Ataangara huyu anayemtazama/Na hakuna haya usoni pake.
6. Maskini akilia,Yahwe amsikiliza/ Na kumwokoa katika tabu zake zote.

7. Malaika ya Yahwe apenda kupanga,karibu na waamini wake: anawakinga.
8. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho,kama mwanzo na daima na milele Amen.

## MBALI YA BWANA, NASHURULIKA. Zaburi 33.

Kiitikio: Mbali ya Bwana,nashurulika! Mbali ya Bwana,hakuna furaha Ee Uje,Mungu mpenzi,uje uje ee, pamoja nawe ee ntatembea.

1. Ulimi wako usitaje mabaya,midomo isiseme maneno ya udanganyifu.
2. Yahwe huelekea macho yake kwa wenyi haki,masikio yake huelekea maombi yao.
3. Wanapolia,Yahwe asikiliza,na kuyaondoa mahangaiko yao yote.
4. Yahwe ni karibu ya nyoyo zinazovunjika,anaponya roho zinazosikitika.
5. Mwamini apigwa na hasara nyingi,lakini Yahwe amkomboa kwa vyote.
6. Mwovu atauawa na ubaya wake,atakayemchukia mwamini atalipa.
7. Yahwe aokoa roho ya mtumishi wake,anayekaa kwake hata pewa malipo.
8. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho,kama mwanzo na daima na milele Amen.

## KAMA PONGO. Zaburi, 41.

Kiitikio: Kichwa changu chajilaza moyoni mwa Rabi,ndipo najaliwa utamu wa mapendo.

1. Kama pongo anayetamani sana maji angavu ya mito,ndipo moyo wangu wakutamani ee Mungu.
2. Nafsi yangu inamwonea kiu Mungu wangu mzima,nisikawiye kumwendea na kusimama usoni pake.
3. Machozi yangu yamenishibisha mchana na usiku,naambiwa bila kituo yu wapi Mungu wako.
4.

4. Hapo moyo wangu hukumbuka siku za matulizo,nipowaongoza makundi ya watu nyumbani mwa Mungu.
5. Niiregee moyoni mwangu nimtumaini Mungu,nimsifu aliye wokovu wangu na Mungu wangu.
6. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho,kama mwanzo na daima na milele Amen.

## USO WAKO MZURI BORA. Zaburi 44.

Kiitikio:Usowako,mzuri bora,Bibi arusi,na ndani yako hakuna kilema.

1. Usikie Binti,utazame,uelekee sikio lako,uwasahau watu wako na nyumba ya babao.
2. Naye mfalme atasangaa kwa uzuri wako,Ndiye Bwana wako,nawe uiname mbele yake.
3. Binti wa Tiro atakutolea zawadi,na watu watajiri watajipendekeza kwako.
4. Mzuri ajabu binti yake mfalme;mavazi yake yamefunikiwa zahabu.
5. Ndivyo atakavyopelekwa kwa mfalme,na mavazi yaliyofumwa kwa hariri nzuri.
6. Wanamwali wenzake wanamsindikiza,wote pamoja wataletwa kwako.
7. Wanakaribia kwa furaha na shangwe,ndivyo wanavyoingia nyumbani pa mfalme.
8. Pahali pa baba zako,watasimama watoto wako,utawapatia ukuu katika inchi zote.
9. Nitalidumisha jina lako katika kizazi na kizazi,ndivyo mataifa watakavyokusifu milele na milele.
10. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho,kama mwanzo na daima na milele Amen.

## KARIBU NA MUNGU  Zaburi 53

Kiitikio: Karibu na Mungu napata raha,na moyo wangu salama.

1. Ee Mungu kwa jina lako uniokoe,na kwa uwezo wako unifanyie hukumu.
2. Ee Mungu uyasikilize maombi yangu,uyasikilize maneno ya kinwa changu.
3. Kwa maana wenyi kiburi wamenishambulia,hawakumweka Mungu mbele yao.
4. Lakini Mungu ndiye anayenisaidia,Bwana ndiye anayenitegemeza nafsi yangu.
5. Atawarudishia adui zangu ubaya wao,na kuwaangamiza kwa uaminifu wake.
6. Kwa ukunjufu wa moyo nitakutolea sadaka,ee Bwana nitalishukuru jina lako maana ni je.
7. Kwa kuwa limeniokoa kwa kila taabu,na jicho langu utazama hodari adui zangu.
8. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho,kama mwanzo na daima na milele Amen.

## NAFSI YANGU YAKUKIMBILIA  Zab. 62.

Kiitikio: Kwako Bwana moyo wangu,hukimbilia daima napenda kujitegemea kuumeni kwako,ee Bwana.

1. Ee Mungu ndiwe Mungu wangu nakutafuta,moyo wangu huona kiu kukupata.
2. Nafsi yangu inakutamani sana,sawa inchi kavu inayokosa maji.
3. Natamani kukutazama pahali patakatifu,kuona uwezo wako na utukufu wako.
4. Mapendo yako ni mema kuliko uzima,kinywa changu kitakusifu.
5. Nitakubariki maishani mwangu,kuinua mikono kwa kusifu lako jina.
6.

6. Ninapokukumbuka kitandani mwangu,nazidi kukufikiria katika maisha.
7. Kwa sababu umekuwa msaada wangu,nafurahi katika kivuli cha mabawa yako.
8. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho,kama mwanzo na daima na milele Amen.

## TUZISIMULIE SIFA ZAKE BWANA. Zaburi 78.

Kiitikio: Tuzisimulie sifa zake Bwana,tuzisimulie sifa zake Bwana, kizazi kwa kizazi.

1. Ee Mungu mataifa wameshika urisi wako,wamechafua hekalu lako, wameharibu Yerusalemi.
2. Wameziacha maiti za watumishi wako,ziwe chakula za ndege za anga.
3. Miili ya waamini wako imekuwa chakula cha nyama wa inchi.
4. Sawa maji,wamemwaga damu yao Yerusalem,pasipo kuwa na mtu kuwazika.
5. Tumetukanwa na jirani zetu,hata wenzetu watuchukia,watuchekelea.
6. Hata lini Bwana utadumu kutukasirikia,hata lini asira yako itawaka sawa moto.
7. Ukali wako uwapige mataifa wasiokujua,Na falme zisizotaja lako jina.
8. Usituazibu kwa ajili ya maovu ya babetu,twajaliwa uchungu, utujie na rehema zako.
9; Ee Mungu wa wokovu wetu,utusaidie,kwa ajili ya utukufu wa jina lako.
10. Usifunge sikio kwa malalamiko ya wafungwa,kwa nguvu ya mkono wako uwakinge hatarini.
11. Nasi wateule wako na kondoo za u nyika wako,tutakushukuru milele na milele.
12. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho,kama mwanzo na daima na milele Amen.

## MWIMBENI BWANA Zaburi 97.

Kiitikio: Mwimbeni,mwimbeni Bwana wimbo mpya,kwani ametenda mambo ya ajabu,mwimbeni Bwana.

1. Kuumeni kwake twaona wokovu,mkono wake wakulia ni mtakatifu.
2. Bwana amejulisha wokovu wake,machoni pa mataifa amefumbua haki zake.
3. Amezikumbuka rehema zake,na uaminifu wake kwa nyumba ya Israël
4. Hata duniani kote hujulikana,ginsi Mungu wetu anavyookoa.
5. Mshangilieni Bwana inchini zote,palizeni sauti imbeni kwa furaha.
6. Mwimbieni Bwana nyimbo kwa kinubi,kwa kinubi imbeni zaburi.
7. Kwa sauti ya tarumpeta,ya baragumu,shangilieni mfalme wa milele.
8. Bahari ivume na vyote vilivyomo,ulimwengu na vyote vikaamo.
9. Mito ipigepige shangwe,nayo milima iimbe kwa furaha.
11. Anahukumu inchi kwa haki,na mataifa kwa adili.
12. Atukuzwe baba na mwana na Roho,kama mwanzo na daima na milele Amen.

## SIFA MUNGU MILELE Zaburi 102.

Kiitikio: Ee moyo wangu,umtukuze Rabi,na vyote vilivyomo ndani yangu visifu jina lake takatifu.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. Ee moyo wangu umtukuze Rabi | Sifa | Mungu | milele. |
| wala usisahau fazili zake zote | " | " | " |
| 2. Akusamehe maovu yote | " | " | " |
| Akuponya bado magonjwa yako yote | " | " | " |
| 3. Akulinda usianguke kaburini | " | " | " |
| Akutia maji ya fazili na rehema | " | " | " |

4. Aushibisha mema uzee wako — Sifa Mungu milele.
Ujana wako hurejea kama tai " " "
5. Bwana afanya mambo ya haki " " "
Na huku njema kwa wanaoonewa " " "
6. Alimjulisha Musa njia zake " " "
Wana wa Israël matendo yake bora " " "
7. Bwana amejaa huruma na neema " " "
Mpole kwa hasira,mwepesi kwa fazili " " "
8. Hagombezi bila kituo " " "
Wala hadumishi hasira yake kamwe " " "

## TOKA CHINI NAKULILIA (De Profundis) Zab. 129

Kiitikio: Nakulilia,ee Rabi mwema,sikio lako Baba,lipokee kwa haraka sauti ya kiumbe chako.

1. Toka chini,nakulilia ee Rabi yangu/ Ee Rabi usikie yangu sauti.
2. Masikio yako yasikilize vema/ Sauti ya kusihi kwangu.
3. Ukikumbuka makosa ee Rabi/ Nani atakayesimama.
4. Kwako lakini maondoleo ya zambi/ Ndivyo utakavyotumikiwa kwa uchaji.
5. Namtumaini yangu Rabi/ Na roho yangu inatumaini lake neno.
6. Roho yangu inamungoja Rabi/ Kuliko wakesha wangojao asubui.
7. Kuliko wakesha wangojao asubui/ Israëli imungoje Rabi.
8. Kwake Rabi yapo maondoleo/ Na wokovu mwingi u kwake.
9. Naye mwenyewe ataiokoa Israëli/ Katika maovu yake yote.
10. Wapumzike na amani katika mema ya Rabi/Na mwanga wa milele uwaangazie.

Archivio Salesiano Roma

## SHUKRANI KWA RABI Zaburi 102.

Kiitikio: Shukrani kwa Rabi,Shukrani,shukrani,mfazili wa wanadamu, Shukrani,shukrani,awashibisha wanao mapenzi mema.

1. Kadiri mbingu ziliinuka juu ya inchi,ndivyo wema wake ni mkuu kwa wamchao;Kama mashariki ilivyombali ya mangaribi,ndivyo alivyoweka zambi zetu mbali nasi.
2. Sawa ginsi baba awahurumia wake watoto,ndivyo Bwana anavyowahurumia wamchao,kwani yeye anatujua umbo letu,akumbuka ya kwamba tu mavumbi.
3. Mwanadamu siku zake ni kama majani,asitawi sawa majani ya unyika,Upepo ukapita juu yake,kumbe afutika na mahali alipo hapamjui tena.
4. Wema wake Bwana wadumu milele kwa wamchao,na pia hurumae kwa watoto wa wanao. Kwa wale washikao agano lake,na kuzikumbuka amri zake,ili wazifuate.
5. Mwenyezi ameweka kiti chake mbinguni,na ufalme unavitawala vitu vyote,mtukuzeni Bwana enyi malaika yake,ninyi mulio hodari mtendao neno lake.
6. Mtukuzeni Bwana enyi majeshi yake,ninyi watumishi mfanyao mapenzi yake; Atukuzwe Baba na Mwana na Roho,kama mwanzo na daima na milele. Amen.

## NYUMBANI KWA BWANA Zaburi 121.

Kiitikio: Nyumbani kwa Bwana,nyumbani kwa Bwana,najaliwa heri amani na furaha.

1. Nalifurahi sana waliponiambia,na twende nyumbani kwa Bwana.
2. Hapo miguu yetu imesimama,milangoni kwako ee Yerusalemi.
3. Ewe,Yerusalemi umejengwa kweli,kama mji ambao sehemu zake zimeshika mana.
4. Huko ndiko wanapopanda makabila,makabila ya Bwana wa milele.

5. Ndivyo wanavyoifuata sheria ya Israëli,walioshukuru jina la Bwana.
6. Kwani huko viwe kwako viti vya hukumu,viti vya nyumba ya Daudi.
7. Ombeni amani pa Yerusalemi,amani ishike wakupendao
8. Amani iwekwe kutani kwako,na pia ndani ya majumba yako.
9. Kwa ajili ya ndugu na rafiki zangu,niseme sasa amani ikae nawe.
10. Kwa ajili ya nyumba ya Bwana Mungu wetu,nakutakia heri na mema.
11. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho,Kama mwanzo na daima na milele Amen.

## UNIOKOE BWANA Zaburi I08

Kiitikio: Uniokoe Bwana uniokoe ! Wema wa Bwana hauna mipaka moyoni pake nima tuteke uwingi wa neema.

1. Kwa ajili ya jina lako unifazili bwana/Kwani wema wako ni mkubwa uniokoe.
2. Mimi mnyonge namhitaji vingi/Na moyo wangu umejeruhi ndani yangu.
3. Ninapita sawa kivulini kiendacho kutoweka/Ninapeperushwa sawa nzige.
4. Magoti yangu yaregea kwa kufunga kwangu/ndivyo pia mwili wangu umekonda.
5. Maadui yangu wanilaumu/Wanitazama wakisukuma kichwa.
6. Ee Mungu wa milele,unisaidie,uniokoe kwa ajili ya wema wako.
7. Nao wajue kama ndiyo mkono wako,ndiwe Bwana umefanya vyote.
8. Wajapolaani wewe utabariki/Wakaidi wataaibishwa,bali mtumishi wako atafurahi.

9. Washambulizi wangu watavikwa fezeha/Watajivika aibu yao kama na joho.
10. Nitamshukuru Bwana kwa kinywa changu/Na kutangaza sifae kati ya wanadamu.
11. Bwana wa milele asimama kuumeni mwa mhitaji/Amwokoa mikononi mwa wanaomhukumu.
12. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho,kama mwanzo na daima na milele Amen.

## KATIKA KIVULI CHA BWANA Zaburi 120.

Kiitikio: Katika kivuli cha Bwana,nafsi yangu hutembea salama.

1. Nainua macho nitazame milima;msaada wangu utatoka wapi.
2. Msaada wangu ni katika Bwana,aliyeumba mbingu na inchi.
3. Hatakubali miguu yangu iregee,hatasinzia Bwana anapomlinda.
4. Hakika hasinzii wala halali usingizi,anayelinda wana wa Israëli.
5. Bwana adumu kukulinda,ndiye kivuli chako kuumeni kwako.
6. Jua halitakupiga mchana,wala mwezi wakti wa usiku.
7. Bwana atatulinda na mabaya yoyote,atalinda roho yako.
8. Bwana atakulinda utakapo na uingiapo,tangu sasa na hata milele.
9. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho,kama mwanzo na daima na milele Amen.

## BWANA ASIPOJENGA. Zaburi 126.

Kiitikio: Usipotenda kwa ajili ya Bwana,mazao ya kazi yako upotea milele.

1. Bwana asipoijenga nyumba,wajengaji wafanya kazi bure.
2. Bwana asipoilinda mji,wenyi kuilinda wakesha bure.
3. Kazi yenu ni bure mukiamka mapema,na kukawiya kwenda kulala.

4. Ndivyo munavyomeza chakula cha tabu,Bwana anapowapa wapenzi wake usingizini.
5. Tazama:waana ndiyo urisi wa Bwana,uzao wa tumbo ndiyo zawadi
6. Sawa mishale mikononi mwa mtu hodari,ndivyo walivyowana wa vijana.
7. Heri mtu aliyejaza mfuko wake,na mishale mingi ya namna hii.
8. Hatashindwa kweli barazani,atakapochongewa na adui zake.
9. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho,kama mwanzo na daima na milele Amen.

## HURUMA YAKE RABI Zaburi 135

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. Tumsifu Rabi kwani yu mwema | HURUMA | YAKE | HUWAKA | MILELE |
| " " Mungu wa miungu | " | " | " | " |
| " " Bwana wa ma Bwana | " | " | " | " |
| 2. Mwenyewe Rabi atutendea maajabu | " | " | " | " |
| Kwa hekimae aliumba anga | " | " | " | " |
| Amezitenga bara na bahari | " | " | " | " |
| 3. Ameumba mianga imerremetayo angani | " | " | " | " |
| Jua limetiwa mfalme wa mchana | " | " | " | " |
| Mwezi umetiwa mfalme wa usiku | " | " | " | " |
| 4. Amewaazibu wamisri wakaidi | " | " | " | " |
| Amewaokoa WaIsraeli mikononi mwao | " | " | " | " |
| Ajulishe hivyo uhadilifu wake | " | " | " | " |
| 5. Amekata njia baharini | " | " | " | " |
| Ili Waisraeli wapitie ngambo | " | " | " | " |
| Firaoni na lake jeshi wamezamamo | " | " | " | " |
| 6. Ametutazama tuliponyenyekea | " | " | " | " |
| Ametuponya mikononi mwa adui | " | " | " | " |
| Ametulisha hoda tu hodarike | " | " | " | " |

Kiitikio: Akuza mnyofu,ashusha mwovu,arudisha zizini kikondoo kilipotevu.

## REHEMA ZA YAHWE Zaburi 127

Kiitikio: Rehema za Yahwe hudumu kizazi,hata kizazi kwa hao wanaomcha.

1. Heri mtu amchae Mungu milele,na kutembea katika njia zake.
2. Ndivyo utakavyokula mavuno ya mkono wako,utaonja heri na maendeleo.
3. Bibi wako ni kama mzabibu uzao sana,katika nyumba yako.
4. Wanao ni kama miche ya mizeituni,kandokando ya meza yako.
5. Ndivyo hivyo atakavyobarikiwa,yule amchae Bwana milele.
6. Bwana akubariki tokea Sioni,uone daima heri ya Yerusalemi.
7. Kumbe ataona wana wa wanao,imani ikae katika Israëli.
8. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho,kama mwanzo na daima na milele Amen.

## SHANGWE KWA BWANA. Zaburi 150

Kiitikio: Allelua,shangwe kuu kwa Bwana Mungu wa milele,allelua allelua.

1. Msifuni Mungu kanisani kwake,msifuni angani penyi ezi yake.
2. Msifuni kwa matendo yake makuu,msifuni kwa ajili ya ukuu wake.
3. Msifuni kwa kilio cha baragumu,msifuni kwa kinanda na kwa kinubi.
4. Msifuni kwa matari na michezo mizuri,msifuni kwa zeze na kwa kinubi.
5. Msifuni kwa matoasi yaliayo,msifuni kwa matoasi yavumayo sana.
6. Vyote vilivyo na pumzi,vimsifu Bwana wetu milele.
7. Sifa kwa Baba , Mwana na Roho,kama mwanzo na daima na milele Amen.

## NINAPOTANGATANGA,UNINYOSHEE MKONO. Zab. 12

Kiitikio: Ninapotangatanga,mbali ya njia zako,
usiniache Yahwe,uninyoshee mkono.

1. Hatalini Yahwe,utanisahau hata mwisho,hataliniutanifichia uso wako.
2. Hata lini roho yangu itakubalia ukaidi,na moyo wangu hujaa huzuni kutwa kucha.
3. Hata lini adui yangu atanisumbua,utazame unijibie Yahwe Mungu wangu.
4. Uangazie macho yangu nisilale kifoni,adui yangu asiseme ninamshinda.
5. Washambulizi wangu wasifurahi ninaporegea,najitolea katika mapendo yako ee Bwana.
6. Moyo wangu ushangilie katika wokovu wako,nimwimbie Yahwe kwa wema alionitendea.
7. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho,kama mwanzo na daima na milele Amen.

## UKWELI WASTAHILI BARAKA. Zaburi 11

Kiitikio: Maneno ya ukweli(ukweli)yastahili baraka (baraka) heri
Ole mwenyi uongo (uongo) achukiwa na Bwana.

1. Uokoe Yahwe,wamcha Mungu hupunguka sana,hakuna haki tena kati ya wanadamu.
2. Kati yao wapenda kusemeana uongo,kwa midomo yao midanganyifu kwa moyo wa hila.
3. Yahwe akatae midomo ya ubembelezi,ulimi mwenyi maneno ya majivuno.
4. Atoe wanaosema,kwa ulimi wetu tutashinda,midomo yetu ni yetu Bwana gani juu yetu.
5. Kwa ajili ya maskini kuibiwa,na mhitaji kulalamika,Yahwe hujulisha:nisimamem hima.
6.

6. Mimi sitakosa kuwapatia wokovu,hawa wote wenyi kutamani sana.
7. Maneno yao ndio ya ukweli,sawa feza la udongoni na iliotakata mara saba.
8. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho,kama mwanzo na daima na milele Amen.

## VIJANA WATATU KATIKA TANURU Danieli 3/52-54-56.

Kiitikio: Tupige shangwe kuu,tupige kelele kwa Mungu wa milele Tumtolee nyimbo nzuri,kwa kinanda,kwa filimbi,kwa zeze kwa matari.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. Usifiwe, Bwana Mungu wa Babetu | Utukuzwe | ushangiliwe | milele. |
| Lisifiwe jina lako tukufu na takatifu | " | " | " |
| 2. Usifiwe hekaluni mwa utukufu mwako | " | " | " |
| Usifiwe kitini mwa ufalme mwako | " | " | " |
| 3. Usifiwe Bwana unaye uwezo juu ya makerubini | | " | " |
| Usifiwe milele mbinguni juu. | " | " | " |
| 4. Usifiwe na milima na mabonde | " | " | " |
| Usifiwe na bara na bahari | " | " | " |
| 5. Usifiwe daima na wanadamu | " | " | " |
| Usifiwe na watakatifu na malaika | " | " | " |

## UTUKUZWE BWANA WE Zaburi 18.

Kiitikio: Utukuzwe Bwana we,mbinguni na duniani usifiwe,Bwana we watu wote wakupende Bwana mwema.

1. Sheria ya Bwana ni kamilifu,aifuatay e husabitishwa roho.
2. Ushuda wa Bwana ni ya kweli,humtilia mjinga hekima.
3. Amri za Bwana ni adili zina furahisha kweli moyo.
4. Amri za Bwana ni adili,safi zinaangazia macho nuru.
5. Kicho cha Bwana ni kitakatifu,kinadumu milele na milele.

6. Ukumu za Bwana ni za ukweli,na zina haki daima.
7. Maneno yake hutamaniwa kuliko zahabu,kuliko zahabu safi bora.
8. Maneno yake ni matamu kuliko asali,kuliko;sega ya asali bora.
9. Kwa hivyo mwamini apenda kuyashika,ndivyo kwa kuyafuata apewa baraka.
10. Atukuzwe Baba na Mwana,na Roho,kama mwanzo na daima na milele Amen.

## KENGELE ZA JUU.

1. Zanena siku kuu,Kengele za juu;waumini furahini,mkombozi mkubusheni,mzawa leo Betlehem,mzawa leo Betlehem.
2. Ni leo siku njema,siku ya salama,aliposhuka Mwokozi,Mwanae Mungu Mwenyezi,kuwa Mwana-Adamu.
3. Siku hii,tuna neema,yameshuka mema,asifiwe Mungu juu,watu wa imani kuu,waletewa amani.

## KIMYA BARA.

Kiitikio: Kimya,kimya,asinzia mpenzi wetu,mtoto Yesu.

1. Kimya bara na bahari,kimya mbingu na dunia,Bwana na muumba wenu, mtoto Yesu asinzia.
2. Amelazwa manyasini,mchanga mkiwa mnyonge pia,Yosef na Maria wamo,mtoto Yesu kumtunzia.
3. Malaika wanashuka,mfalme wao kumlindia,wanatunga nyimbo nzuri, mtoto Yesu kumwimbia.
4. Nasi pia twende hima,Mungu wetu kumwangalia,twende wote kwa juhudi,mtoto Yesu kuamkia.

## MBALI KULE

Kiitikio: Glooooooria in excelsis Deo ! Glooooooria in excelsis Deo.

1. Mbali kule nasikia, malaika wa mbinguni, wakiimba wengi pia, wimbo huyu jû angani.
2. Wachunga tuambieni, sababu ya nyimbo hizo, mwenyi kuimbiwa ni nani, jû ya nani sifa hizo.
3. Je hamjui jambo kuu, ka kuzaliwa Mwokozi, habari ya wimbo huu, ndizo kumshukuru Mwenyezi,
4. Kweli nasi twende hima, tufike kule aliko, tuone mtoto na Mama tuwasalimie huko.

## LALA KITOTO CHA MUNGU.

Kiitikio: Lala kitoto cha mbingu, sinzia Mwana wa Mungu, Lala, lala, Mwana Yesu lala.

1. Lala kitoto cha mbingu, ndûwetu sinzia, Malaika wake Mungu, watakutunzia.
2. Bikira Maria Mama, kambusu Mwanae, kamlaza nyasini vema, kamshika mkononwe.
3. Yosef kasimama pale pale, Baba mlishi mwema, mnye kumtunza mtoto kule pamoja na Mama.
4. Nasi sote tumwendee Mwana wake Mungu; maamkio tumtolee, atokaye mbingu.

## HODI WACHUNGA.

1. Hodi wachunga, musiwe na woga, amukeni upesi, Betlehem muje nasi alipozaliwa Mwokozi wenu.
2. Hayo, twendeni huko mpangoni; Nyasi akalia, aliwashukia Mwenyezi wa mbingu, Mwokozi wenu.

3. Pamoja naye muna Mamae,Yeye na Yusufu,mlinziwe mtukufu,wamtunza kitoto Mwokozi wenu.
4. Mtukufu Mungu katika mbingu,na kwenu amani kwa watu amini, wenyi kumwungama Mwokozi wetu.
5. Wakristu nyie,twende nasiye kwenye Mwana mchanga kamao wachunga: nasi tumwabudu Mwokozi wetu.

## GLORIA,SIFA KWAKE MUNGU.

Kiitikio: Gloria,gloria,gloria,sifa kwake Mungu na amani duniani kote kwa wamchao Mungu.

1. Kila amchae Mungu aimbe sifa yake,kwani leo Mwokozi amezaliwa.
2. Mwokozi huyu ni nani,ni Mwana wa Mungu,aliyetuadiwa tangu zamani za kale.
3. Atuletea nini,atuletea amani,mapendo ukweli,umoja undugu pasipo mwisho.

## USHUKIE MASIHA.

Kiitikio: Ushukie Masiha,kuaokoa watumwao,mokombozi Masiha, Njoo,njoo,njoo.

1. Shuka kwetu sikawiye,twapotea tuokoe hima,hima tusashie.
2. Tangu zambi ya wazee,twakungoja utuokoe,kwetu hapa tushushie.
3. Ni kifano chake Mungu,sizaifu Roho yangu,yatamani ya uwingu, kumefungwa lakini yamepigwa makatao,tusiingiie ndani,njoo,njoo, njoo.
4. Siwe tena uso mkali angalia yetu hali,twelekee sasa kweli: Mashetani huwaka vita nzito tuna leo,ulimwinguni shuka,njoo, njoo,njoo.
5. Waja wako walilia,mali bora kupotea,twatamani kurejea,yatutoka machozi,tukiomba rehemayo,tuwilie razi,njoo,njoo,njoo.

Archivio Saveriano Roma

## SASA LATIMIA.

Kiitikio: Sasa latimia, sasa latimia agano alilosema tangu kale sasa latimia.

1. Usiku kati nasikia sauti tangu mbali sana Malaika wote waja wakiimba, sasa latimia.
2. Herodi mfalme wa Galileya alietafuta Roho yake Misri akaenda baba akamlinda.
3. Wachunga waliobondeni njooni wote kwa haraka kitoto maskini chalazwa nyasini.
4. Maria akamfunika Yusufu akamchungulia, kwa msangao wote, wote wakaimba.
5. Wakwanza nani kuabudu Majusi waliotoka mbali alama ya nyota ikawatangulia.

## AHADI YA MUNGU IMETIMIA.

Kiitikio: Ahadi ya Mungu imetimia allelua, yukati yetu Emmanueli allelua, allelua, allelua, allelua.

1. Twende tukamwone Mwana tumtolee sadaka zetu, umaskini wa roho na wa mwili.
2. Wangambo zote za dunia, waweza kumwona, bila ubaguzi wa kabila ao wa rangi.

## AVE MARIA.

Kiitikio: Ave, ave, ave Maria, ave, ave, ave Maria.

1. Bikira Maria anaelezwa ya kama atakuwa mama wa Yesu.
2. Bikira Maria anasafiri, kwenda kumlaki Elisabeth.
3. Bikira Maria pa Betlehem, Mtoto amezaliwa mkombozi wetu.
4. Bikira Maria anamtolea, mu hekalu la Mungu kitoto Yesu.
5. Bikira Maria anamkuta Yesu, mu hekalu la Mungu pa Yerusalem.

## MUUMBA JUA NA NYOTA.

1. Muumba jua na nyota anga la watu amini;Yesu mkombozi,Masiha utuelekee waombi.
2. Udanganyi wa shetani motoni usitubwage kwa mapendo kwetu sisi, umekuja utuponye.
3. Kutuondolea upate,wazaliwa na Bikira,japo simzambi mweupe, mtini wafa sadaka.
4. Basi leo twakungoja ee mwamzi mkuu wa mwisho,utukingie kwa neema mwovu tupate mzarau.
5. Ndiwe mwenyi utukufu,Mungu Baba na Mwanae,naye Roho Mtakatifu leo kesho na milele.

## TUKIPENDA WENZETU

Kiitikio: Tukipenda wenzetu,kati yetu Mungu yuko.

1. Aliyetufanya tuwe ndugu,ndiye Yesu ndugu yetu,chuki yote na hasira kati yetu ziondoke.
2. Tukipenda Mungu wetu kweli,tuanzie na nduguze,auzie moja wao mapendoyo si ya kweli.
3. Tuwe roho moja moyo moja,tuwe pia kundi moja,tupendane kama vile Yesu alivyotupenda.
4. Furahini nyote Binadamu,mwimbieni Mungu wetu,amri yake ni nyepesi,neno lake kupendana.
5. Kati ya ugonvi na fitina,na katika kisilani,Mungu wetu hapapendi Mungu wetu wa amani.
6. Yesu kiongozi wetu mwema,amri yako twaijua,washa nyoyo ya Wakristu,wapendane siku zote.

## HUO NDIO NI MWANZO.

Kiitikio: Huo ndio ni mwanzo wa Ufalme wa Mungu.

1. Umpende Mungu kwa moyo wote,maana ndiye Baba yako.
2. Umtendee mwenzako,upendavyo kutendewa naye.
3. Ujikaze kila siku,uchukue vema msalaba wako.
4. Heri ukiwa maskini moyoni,maana ufalme wa mbingu ni wako.
5. Heri ukiwa mpole,maana utapata inchi.
6. Heri ukiona uzuni;maana utatulizwa.
7. Heri ukiona njaa ya kupata utakatifu,maana utashibishwa.
8. Heri ukiwa na huruma,maana utahurumiwa.
9. Heri ukiwa na moyo safi,maana utamwona Mungu.
10. Heri ukipenda amani,maana utaitwa mwana wa Mungu.
11. Heri ukisumbuliwa kwa ajili yangu,maana tuzo lako litakuwa kubwa.
12. Heri ukiukubali,kila siku ya maisha.

## AKSANTI SANA YESU.

Kiitikio: Sisi watoto wako wapenzi mno,twakuomba huruma tupatie.

1. Aksanti sana Yesu,aksanti sana Yesu.
2. " " " kwa neema zako zote.
3. " " " kwa mema yako yote.
4. " " " kwa wazaa wetu wote.
5. " " " kwa marafiki wetu.
6. " " " kwa wakubwa wengine.
7. " " " kwa wasiotupenda.
8. " " " huruma kwa wazaifu.

Archivio Storico Roma

## TUNAPOKEA MUNGU.

Kiitikio: Tunapokea Mungu mwenyi uzima,na moyo wetu unajaa na furaha.

1. Nipo mkate,unayotayarishwa kwa chakula chenu.
2. Nipo uzima,nashinda kufa.
3. Nipo njia,ya kwenda karibu na baba yangu.
4. Nipo mapendo,yanayokusanya watu wote.
5. Nipo amani,katika masumbuko ya dunia.
6. Nipo mwana kondoo aliyekufa kwa watu wote.
7. Nipo nguvu katika uzaifu wenu.
8. Nipo ukweli,wenyi kunisadiki wataishi.
9. Nipo mfalme,wa mataifa yote ya dunia.
10. Nipo mchungaji mwema,najua kondoo zangu nazo wanijua.

## TUPO WAKRISTU

Kiitikio: Tupo wakristu watoto wa Mungu,tupo wakristu kwa milele.

1. We shetani mbaya sana,tunakukataa kabisa,tupo wakristu kwa milele.
2. Tutatunza dini letu,siku zote za uzima wetu,tupo wakristu kwa "
3. Mungu ni Baba yetu,tutamfuata kabisa,tupo wakristu kwa milele.
4. Yesu Kristu ni mwokozi,yupo pia mfalme wetu,tupo wakristu kwa......
5. Eklezya mama yetu,tutabaki waamini kwako,tupo wakristu kwa........
6. Sifa kwa Baba na Mwana,pia kwako Roho mtakatifu,tupo wakristu kwa..

Tupo wakristu kwa milele.
Ni heri yetu kwa milele.
maisha yetu kwa milele.
tutamwekea kwa milele.
Mama Eklezya kwa milele.
tukaupate kwa milele
ukomo wetu kwa milele
juu mbinguni kwa milele.

Archivio Saveriano Roma

## SHUKURUNI MUNGU.

Kiitikio: Kwani huruma yake ndiyo ya milele.

1. Shukurini Mungu kwani ndiye mwema.
2. Shukuruni Mungu ye mkubwa wa Myungu.
3. Niye akafanya miujiza mingi.
4. Niye akaumba mbingu kwa hekima.
5. Katia udongo mkavu juu ya maji.
6. Ni ye akafanya myanga hii mikubwa.
7. Akatia jua liangaze mchana.
8. Mwezi nazo nyota,ziangaze usiku.
9. Kawapiga wana wa kwanza wa Misri.
10. Katoa Israel kati ya wa Misri.
11. Na kwa mkono wake wa nguvu kabisa.
12. Kayatenga maji bahari jekundu.
13. Kawapiga hapo wana Israeli.
14. Farao na jeshi kumwanga majini.
15. Na kabila lake kaleta jangwani.
16. Kawapiga pia sultani jangwani.
17. Na kaangamiza sultani wakali.
18. Sehon mfalme kauwawa pia.
19. Naye inchi nakampa Israël
20. Akakumbukia umaskini wetu.
21. Akatuokoa kwa adui zetu.
22. Ni ye analeta chakula kwa wote.
23. Shukuruni Mungu wa mbingu Babetu.

Archivio Generale Saveriano Roma

## KUBARIKI NA KUGAWANYA MATAWI.

Hosana kwa Mwana wa Daudi,mbarikiwa mwenyi kuja kwa jina la Bwana: Ee mfalme wa Israëli: Hosana juu mbinguni.
Waana wa Mayaudi,walitandika mavazi njiani,wakimwimbia Bwana na kusema: Hosana kwa Mwana wa Daudi mbarikiwa mwenyi kuja kwa jina la Bwana.

## UTUKUFU SIFA NA HESHIMA.

Kiitikio: Utukufu sifa na heshima kwako,ee Kristu mfalme Mkombozi watoto walikuimbia kwa mapendo wimbo wa Hosana.

1. Wewe ndiye mfalme wa Israëli na mwana mkuu wa Daudi,ee mfalme mbarikiwa unayekuja kwa jina la Bwana.
2. Malaika wa mbinguni wanakusifu na watu wa ulimwengu wote wanakushangilia pamoja.
3. Mayaudi wanakufikia kwa matawi,na sisi tunakuja kwako kwa sala, maombi na nyimbo.
4. Wakakutolea heshima mbele ya kufa kwako,Sisi tunakuimbia ukiwa katika utukufu Mbinguni.
5. Nyimbo zao zikakupendeza,ikupendeze pia ibada yetu,Ee mfalme mwema,mfalme mpole,mema yote yanakupendeza.

## TUMSIFU YESU.

Kiitikio: Tumsifu Yesu,Bwana wetu,tumsifu tumshukuru,asifiwe,asifiwe,asifiwe Mwana wake Mungu.

1. Tumsifu Bwana wetu na Mwokozi wetu/Tumpe nyoyo zetu.
2. Ametukombea utumwani mwa shetani/ Siku zote anatupenda.
3. Ewe mwanga wa wote/ Imani utuletee.
4. Aksanti Yesu kwa wema wako/ Umetuokoa.
5. Kwa mapendo yako/ Umekufa kwa ajili yetu.

6. Ndiwe mwangaza wa wote/ Na mfalme wetu wa kweli.
7. Yesu Mungu na mwangaza/Wapani wamjue Mungu.
8. Utupe huruma nyingi/ We mwenyi huruma nyingi.

## TUPALIZE SAUTI ZETU.

Kiitikio: Zipokee zetu heshima,zipokee zetu nyoyo,zipokee zetu heshima,zipokee zetu nyoyo.

1. Tupalize sauti zetu wote tumtukuze leo,tumtukuze mkombozi wetu: Mpenda kwa watu makao Yesu ndiye mchungaji mwema,twakujua siye wakristu.
2. Wazee wetu wa zamani,sadaka na hutoa,wakifukizia ubani,na nyama wakichinjia,mara akatokea Mwokozi,Acheni kondoo mbali,Babangu hazimpendezi,ndimi sadaka ya kweli.
3. Isipo mtosha msalabani mara moja itolewe,akatwaa mkate mezani, kugeuza mwiliwe;mle hii mwili wangu;Mitume kiwaambia,ndiyo sadaka mpya ya Mungu;nda peke kutufalia.
4. Basi mitume tangu hapo,hutoa sadaka ile,mijini na nchi wapitia-po,kumkumbuka Rabi vile,hata leo kwetu mijini,Padri hutoa sadaka,Yesu hutuka uwinguni,Mpenda kwa watu kushuka.
5. Yesu mkombozi kwa Damuyo,wala hukutusahau,siye watu wa Bara hiyo, ukatutokea leo,Mungu pamwe na Binadamu,mtu-Mungu twakuungamia, twaabudu mwili na Damu,kichwa chini tukiinama.

## EWE YESU.

Kiitikio: Ewe Yesu upokee,nyimbo zetu za sherehe,tujalie mapendoyo twaa zetu nyoyo.

1. Mtoto Yesu mpendelevu,tunakuamkia,ndiwe mzuri mnyenyekevu,mvu-milivu pia.
2. Mtoto Yesu mtoto mpenzi kama maskini umekuja wetu mwenzi Duniani chini.
3. Kwa ajili yetu sisi tuliopotea umeshuka uwinguni kwetu kutuokoa.

4. Yesu tunakushukuru kwa mapendo hayo tujalie neema nuru yote tuombayo.

## MAMA SAFI SANA.

Kiitikio: Mama safi sana we,utuombee kwa mwana wako Yesu,kwani dunia yote ya potea.

1. Kwa Mungu Baba — Huruma
   Kwa Mungu Mwana — Huruma
   Huruma kwa dunia yote.

2. Kwa Roho mtakatifu — huruma
   Utatu mtakatifu — huruma
   huruma kwa dunia yote.

3. Kwa mama wa muumba — huruma
   Bikira wa sifa — huruma
   huruma kwa dunia yote.

4. Mkingwa zambi ya asili — huruma
   Mbarikiwa kuliko wanawake wote
   huruma kwa dunia yote.

5. Tumsifu Mungu — huruma
   Milele na milele — huruma
   huruma kwa dunia yote.

## YESU KUPAA MBINGUNI.

1. Mshinda nguvu za shetani,Yesu kapaa mbinguni,Malaika wote pia wakaja kumshangilia.
2. Tupe Yesu neema yako,tupate kufika kwako,tufae sifu milele wema wako juu kule.
3. Umeshuka chini kwetu kuondoa zambi zetu,ukapaa kwake Mungu utufungulie mbingu.

4. Ee Yesu wetu Mkombozi uwe wetu kiongozi,uwe leo kitulizo uwe kesho letu tuzo.

## KUPAA KWAKE RABI.

Baada siku si nyingi hamtanionako tena mimi (bis)
  Maana ntarudi kwa Baba jû,ntarudi kwa Babangu jû: Ntalia machozi shida mtapata Dunia furaha.
Mitume wake husangaa na kuuliza uchunguni
  Ni **mimi** maneno hayo ni je ?, Ntarudi kwa Babangu jû, Mtalia machozi shida mtapata Dunia furaha.

## TUMEKUJA

1. Tumekuja: Tumekuja kutembea duniani/ Inchi yetu ni mbinguni.
2. Siku moja: Siku moja tarumpeta italia duniani/ Bwana Y.Atashuka.
3. Kuuliza:mafundisho gani mumefanya duniani/Ya mazambi mulioyatenda.
4. Roho yangu:Roho yangu ni kitabu cha kusoma duniani/Ya kujua mabaya na mema.
5. Mama Maria: Mama Maria ni kitabu cha kusoma duniani/Kwa kujua wazima na wafu.
6. Ningefanya:Ningefanya sikitiko timilifu ya imani/Ningefurahiwa pamoja na Baba.
7. Vya dunia:vya dunia vitabaki na duniaaa/Nitarudi kwa Mungu Baba.
8. Mwili wangu:Mwili wangu ni kitu cha kuoza duniani/Na kutupwa ndani ya udongo.
9. Nikifanya: Nikifanya mazambi mu duniaaa/ Nitateswa moto wa jehanama.

Archivio Saveriano Roma

## ASIREGEE MOYOWE.

1. Asiregee moyowe,asitoke machozi,akimkumbuka Mungu we,kwa yake makombozi,mtoa roho msalabani,mtaka kufa mwenyewe,kwa sababu kupendani,nani mfungwa moyowe.
2. Bustani mule Getsemani,amwomba Mungu Baba,je mtu-Mungu ana nini nguvu zake ni haba: Rabi yangu waziona zambi za bin'adamu; mwili wako umetona kama jasho la Damu.
3. Salamu Rabi,Salamu,anenan Yuda mbaya,mwenye moyo wake mgumu ambusu pasi haya. Aliwaambia basi: ntakayembusu ndiye,mtwaeni na kwa upesi,Yuda nani? ni siye.
4. Yuda nani ila yeye aliyetenda zambi akikosa kwa Mungu we,mtenda zambikwa juhudi. Mwenyewe kumtende mema,mtaka zambi haoni kwamba ni kutupa neema,kumwendea shetani.
5. Wote ni kupiga mbio mitumewe pamoja. Wamtia mikono yao askari waliokuja,wampeleka hukumuni,aamuliwe na mtu mnye kutoka Uwinguni,mwamzi mkuu wa watu.
6. Mtume Petri amkanusha amenena simjui,uhodari umekwisha macho yake hainui. Pilati amwona Rabi hakukosa'ta neno,asema sioni zambi,lakini ni mwoga mno.
7. Hasubutu kumwachia,si hukumu aomba:Mmoja nitamfungulia,Yesu ao Baraba;Wayaudi,mwamtakani ? Baraba aachwe tu,Yesu afe msalabani,damu yake juu yetu.
8. Pilati hukumu gani,simo nanawa mkono,mkimtaka Yesu,mwueni. Mara askari wamwanza:ni kupiga kelele,kumcheka na kumchokoza mwenye mama milele.

## MAMA PALE MSALABANI.

1. Mama pale msalabani,macho yatoka machozi,akimwona mwanaye.
2. Kweli vile akilia,uchungu kama upanga,ukampenya moyowe.
3. Mwenye moyo mgumu nani,asimuhurumie basi,Mama mlilia Mwana.
4. Ewe Mama mtakatifu,usulubiwe na Yesu,moyo wangu mwenye zambi.

5. Nae Mwokozi niteswe,na madonda nigawie,pamoja na Mkombozi.
6. Nisimame msalabani,niwe nami wako mwenzi,wa uchungu na msiba.
7. Nisianguke motoni,uniwie msimamizi,ewe Bikira mwema.
8. Msikilize Mama wako,niponye siku za mwisho,Ewe Mwokozi wangu.
9. Nitakapo kufa mimi,ipokee roho basi,niende kwako Mungu.

## BINADAMU INAMA KICHWA.

1. Binadamu inama kichwa,umwabudie Mungu mtu. Hapa yupo ajapo fichwa,ameshuka chini kwetu:Hapa yupo ajapo fichwa,ameshuka chini kwetu.
2. Kwa macho yetu hatuoni,ila maumbo ya mkate,hatuna ta mkate lakini,mwiliwe twarisi sote,
3. Kukaa basi umetaka,Rabi mwema,mpenda watu,kwa tamaa nyoyo, zawaka,njoo basi ndani mwetu,

## TWAKUABUDU MKATE.

Kiitikio: Yesu ! Yesu ! Yesu, Daima mtakatifu,Yesu Mungu wetu daima twakusifu,

1. Twakuabudu mkate wa mbinguni;faraja yetu hapa uchunguni.
2. Twakushukuru,Yesu,kwa wemao;kwa mkate huo na kwa msalabao.
3. Twatubu zambi,Yesu,tusamehe,makosa yetu utuondolee.
4. Twaomba kwako,neema tujalie,e Yesu mwema,utufanyizie.
5. Twatubu zambi,Yesu tusamehe,kwa mkate hû leo tubarikie.

## KIKONDOO CHA MUNGU.

Kiitikio: Kikondoo cha Mungu,mkate wa mbinguni,mlishi wa roho yangu,nakuabudu.

1. U Babangu mwema,na msimamizi,mpaji wa uzima,wangu mwokozi.
2. Fumbo abudiwa na kuamini,kaza Yesu mpendwa yangu imani.
3. Mloa Roho yangu hostia nzima,niwiye ya mbingu kweli amani.
4. E Rabi,Mtu-Mungu unirizishe,njoo shuka kwangu kanishibishe.

5. Anakaribia mpenzi amini,atakaingia mwangu moyoni.

## KUMPENDA YESU.

Kiitikio: Mapenzi yangu e Yesu kupenda daima weye tu.

1. Mwokozi wangu ntakupenda,mapendo bora yakufaa,tamaa yangu ni kutenda,matendo nema kila saa.
2. Nitakupenda e rafiki,Sababu wanipenda mno,memayo hayahesabiki ta umekufa kikondoo.
3. Na miye nalikuwa mpofu,nikafuata zambi tu. Katika wangu upotofu nikazarao wema huu.
4. Lakini sasa narudia,maovu yangu natubu,Nitakupenda e Masiha ! Nitakupenda kweli weye tu.
5. Nakushukuru kwa memayo,naomba kwako nema hî: nitunze makusudi hayo,nikupendeze nikutii.

## ALLELUA BWANA AMEFUFUKA.

Kiitikio: Utukufu wake kwa milele,mbinguni juu pamoja na Baba.

1. Tumjongelee Yesu mtukufu;alleluia Bwana amefufuka.
   Amefufuka katika wafu: alleluia Bwana amefufuka.
2. Mmeona nini ku kaburi: Wewe Magdalena na Salome.
3. Siku tatu kiisha kufa kwake,ametoka peke kaburini.
4. Sasa akuja kwa kutulisha: Mwili wake chakula cha roho.
5. Tukila mwili wake mtukufu: Tutapokea uzima mpya.
6. Mababu wenu wakala mana: Ila njiani wote wakafa.
7. Ila alaaye mwili wangu: Nitampa uzima wa milele.

Archivio Saveriano Roma

## MBINGU INCHI NA BAHARI

Kiitikio: Alleluia,alleluia,alleluia.

1. Mbingu inchi na bahari Alleluia. Tuungane furahini. Alleluia.
2. Tumwimbie Kristu wetu " Mzima kashinda mauti "
3. Sanda zake za mauti " Zangara kama jeluji "
4. Alfajiri Magdalena " Kaburi kaenda hima "
5. Akalikuta ni wazi " Ameketi Malaika "
6. Kweli Bwana yu mzima akanena Malaika "

## TULENI WOTE.

Kiitikio: Tuleni wote,tuleni wote,Tuleni mwili wake na pia,na pia damu ya Bwana Yesu,Tupate,tupate uzima wa milele.

1. Siku ile takatifu,Bwana Yesu mezani,akakamata mukate,akawapa mitume.
2. Na kiisha akatwa,kikombe cha divai,akawapa akisema hii ndiyo damu yangu.
3. Ninawapa amri mpya,pendane nyinyi wote.Kama vile nawapenda kwa mapendo makubwa.
4. Ndani mwako tuna nguvu ya kushinda mabaya,Kama vile ulishinda juu ya sadaka yako.
5. Kwa mwili wako Bwana Yesu,ponya vidonda vyetu.Na pia kwa damu yako safisha roho zetu.
6. Kwa mwili wako Bwana Yesu,uishi ndani mwetu.Tupate kuwa umoja kule mbinguni.

## TUNAKUABUDU YESU ALTARENI.

1. Tunakuabudu Yesu altareni,kwa ajili yetu wajifunga kweli. Tunakufikia e wetu rafiki.
2. Twakusadikia Yesu altareni,na tunakupenda e Yesu mpenzi,utusaidie ee wetu mfazili.

3. Utubarikie Yesu altareni,na utukingie tusitende zambi,ulinde daima ndugu na wazazi.

## NITAJONGEA ALTARE YA BABANGU.

Kiitikio: Nitajongea altare ya babangu/Nitaingia nyumbani mwa Babangu/ Nitajongea altare ya babangu/ Furaha yangu na heri yangu.

1. Napiga hodi kwa Babangu/ Na yeye ananikaribisha/ Na sitatanga-tanga tena/ Nipeperushwe sawa mavumbi.
2. Ee Yahwe Mungu wa majeshi/ Univike mavazi ya chuma/ Unitenge na wachekaji/ Wanauliza ni nani Yahwe.
3. Nasikia sauti nyingi/Zanizunguuka pande zote/ Zanitia na wasiwasi/ Zinivike mavazi ya chuma.

## TUNAENDA KWA BWANA YESU.

Kiitikio: Tunaenda kwa Bwana Yesu/Sisi watoto wako/Tunakupenda sana/ na utulinde kabisa Bwana Yesu/ Na wewe ndiyo kimbilio letu.

1. Ee Bwana tunakufikia upate kuosha moyo wetu/ Na uzidi kutusaidia tufuate amri zako.
2. Mwili wako ni chakula kweli/ Asiyekula mwili wako hana uzima kamwe.
3. Ee Bwana,anaye kula mwili wako anauzima/ Anakaa ndani mwako.
4. Tumsifu Bwana wetu na Mwokozi wetu/ Tumpe myoyo zetu.
5. Nami nitajongea ee Mungu/ Na roho safi na mapendo.
6. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho/ Kama mwanzo na daima na milele Amen.

## UTULISHE.

Kiitikio: Utulishe,utunyweshe,tupate uzima mpya.

1. Ee Mama wetu Maria/Tupatie Yesu wako.
2. Pa regevu tia nguvu/ Penyi taka usafishe.
3. Utupatie uzima / Wa mwili pia wa Roho.
4. Kwa kupata Yesu wako/ Twaomba mama Maria.
5. Utulishe mwili wako/ Utunyweshe damu yako.

## KUMSIFU MUNGU.

Kiitikio: Sifa kwake Mungu alleluia/ Leo siku zote alleluia.

1. Twataka Mungu atawale/ Katika inchi zetu zote.
2. Ufalme wake usimame/ Imani itujalie.
3. Twataka Mungu atawale/ Katika nyoyo za watu.
4. Kishenzi upuuzi waache/ Washike mambo ya Dini.
5. Twataka Mungu atawale/ Katika jamaa zetu.

## MAMBO YA AJABU.

Siku moja Bwana Yesu alimwambia mtu (bis).
Nenda nyumbani mwako ukafundishe ...... Mambo ya ajabu niliowatendea.
Nenda mjini mwako ukahubiri ...... " " " "
Nenda kwa ndugu zako ukatangaze ...... " " " "
Nenda kwa jamaa lako ukaeleze ...... " " " "
Leo vile Bwana Yesu anatuambia:
Mwende nyumbani mwenu mukafundishe ..... " " " "
Mwende mjini mwenu mukahubiri ..... " " " "
Mwende kwa ndugu zenu mukatangaze ..... " " " "
Mwende kwa jamaa lenu mukaeleze ..... " " " "

## UPOKEE SALA ZETU ZOTE.

Kiitikio: Upokee sala zetu zote eee,Mama Maria:
Utulinde humu duniani iii,Mama Maria.

1. Wangalie jamaa lako nzima aaa Bwana Yesu.
   Uwalinde wote na watoto ooo Bwana Yesu.
2. Huyu-ni wimbo wetu wa furaha aaa Mama Maria.
   Utuweke mkono wa kuume eee Mama Maria.
3. Mupunguze vita kali sana aaaa Mama Maria
   Utuweke nia moja sawa aaa Mama Maria.
4. Tuletee heri na amani iii Mama Maria.
   Tunaomba nyinyi wote pia aaa Mama Maria.
5. Tunaomba toba kwako mama aaa Mama Maria.
   Wangalie hali na machozi iii Mama Maria.
6. Mama mwema wangalie wana aaa Mama Maria.
   Wasumbuka duniani hapa aaa Mama Maria.
7. Twatolea nia yetu kwako ooo Mama Maria.
   Ondolea uzaifu wetu uuu Mama Maria.

## POKEA BABA MATOLEO YETU.

Kiitikio: Pokea baba matoleo yetu,ni matunda ya kazi ya wanao.

1. Mkate na divai twakutolea Baba/ Ila ukipenda vitageuka Mungu wetu.
2. Kazi na nguvu zetu twakutolea Bwana/ Tuwe watumishi wakujenga ufalme wako.
3. Magumu na magonjwa twakutolea yote/Utusaidie yatufalie kwa wokovu.
4. Imani yetu ndogo twakutolea yote/ Tupatie neema ya kukamilisha ukristu wetu.
5. Raha na maibha yetu twakutolea Baba/ Twataka kuishi katika mapenzi yako milele.

## POKEA SISI BWANA.

1. Pokea sisi Bwana alleluia, na matoleo yetu, alleluia.
   Tukiungana wote alleluia, tunakukaribia alleluia.
2. Pokea kweli Bwana alleluia magumu yetu yote alleluia.
   Furaha zetu zote alleluia, huzuni zetu zote alleluia.
3. Pokea nguvu zetu, alleluia, na uzaifu wetu alleluia.
   Maisha yetu yote, alleluia, uyapokee kwako, alleluia.
4. Tubarikie sisi, alleluia, wazazi wetu wote alleluia.
   Wabarikiwe pia, alleluia, Dada na kaka zetu alleluia.
5. Vibarikiwe pia, alleluia, vyote viumbe vyako alleluia.
   Na sisi watu wote, alleluia, tufurahiwe nawe, alleluia.
6. Ewe Baba wa mbingu, alleluia, tusaidie sisi, alleluia.
   Kufika kule kwako, alleluia, mbinguni kwa milele, alleluia.

## UKUBALI KUIPOKEA.

Kiitikio: Ukubali kuipokea Baba sadaka hiyo.

1. Kwa mikono ya Yesu Mwanao Pokea sifa.
   Mwenyi kukutolea sadaka " "
2. Kwa imani ya kanisa yako " "
   Na maombi ya mama Maria " "
3. Ya wana wako na watu wote " "
   Ya vitu vyote ulivyoumba " "
4. Ya shangwe na shukrani moyoni " "
   Ya kuabudu na kuomba toba " "
5. Kwa utukufu wa jina lako " "
   Na umoja wa kanisa lako " "

## NINAKUTOKEA MUNGU.

1. Ninakutolea Mungu pamoja na hostia,sadaka ya nafsi yangu, ikupendeze Bwana.
2. Tone la maji ni mfano wa uzaifu wangu,sabitisha yangu roho, najiunga na Yesu.
3. Utujaliee kwa fumbo la maji na divai,tuweze kusharikiana na uMungu wako Bwana.
4. Katika sadaka hiyo,twapenda kuungana,na wakristiani wote,kwa sala na mapendo.

Kiitikio: Kwako tunajitolea,ukubali kupokea,mwili wangu na roho yangu unilinde vema.

## WIMBO WA MATOLEO.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Pokea Bwana zawadi ya wana wako | uipokee,ee | Bwana. |
| 2. | Zawadi yetu n'ile ya mkombozi wetu | " | " |
| 3. | Sadaka ya Yesu ndiyo twakutolea | " | " |
| 4. | Iifalie Eklezya jamaa lako | Utusikie,ee | Bwana. |
| 5. | Imfalie Papa na Maaskofu wetu | " | " |
| 6. | Iwafalie Mapadri na watawa | " | " |
| 7. | Iwafalie wakristu watoto wako | " | " |
| 8. | Iwafalie wote wafuatao dini | " | " |
| 9. | Iwafalie pia wazazi wetu | " | " |
| IO. | Iwafalie wote waliofariki | " | " |
| 11. | Iifalie pia inchi yetu | " | " |
| 12. | Tunakutolea Bwana dunia nzima | Uigeuze ee | Bwana. |

Archivio Saveriano Roma

## BABA MWEMA.

Schola: Baba mwema (bis) wote: Watuona mbele yako kwa kukutolea sadaka yetu.

1. Na nafsi zetu — Pokea Baba twaomba.
2. Maisha yetu — " " "

   Baba mwema watuona mbele yako kwa kukutolea sadaka yetu.
3. Na kazi zetu — Pokea Baba twaomba.
4. Na jamaa zetu — " " "

   Baba mwema watuona mbele yako kwa kukutolea sadaka yetu.
5. Na inchi yetu — Pokea Baba twaomba.
6. Na jimbo letu — " " "
7. Na Mission yetu — " " "

   Baba mwema watuona mbele yako kwa kukutolea sadaka yetu.

## TWENDE KWA MWENYEZI.

Kiitikio: Twende kwa mwenyezi katika nyimbo za shangwe.

1. Dunia nzima ishangilie Rabi/ Kwa furaha tumtumikie wote/ tumwendee na nyimbo za shangwe.
2. Mujue Rabi yetu ni Mungu/ ametufanya na tuko watu wake/ Sisi kondoo za malisho yake.
3. Ingieni mulangoni kwa kumsifu/ Nyumbani mwake tumtolee heshima/ tutukuze jina lake kubwa mno.
4. Kweli Mungu ni mwema sana/ Na huruma yake ni ya milele/ Uaminifu wake kwa vizazi vyote.
5. Utukufu kwa Baba mwenyezi/ na kwa Mwana mwokozi wetu/ Na kwa Roho mtakatifu ndani mwetu.

Archivio Saveriano Roma

## KARIBU YA BWANA.

Schola: Karibu ya Bwana (bis) wote: Nifungue moyo wangu niwe tayari kumpokea.

1. Ufungue moyo wangu Na nguvu yako kaingie.
2. Uuujaze moyo wangu " " "
   Karibu ya Bwana nifungue moyo wangu,niwe tayari kumpokea.
3. Ni tayari roho yangu Na nguvu yako kaingie.
4. Sikitisha roho yangu " " "
   Karibu ya Bwana , nifungue moyo wangu,niwe tayari kumpokea.

## TUMEPEWA AMRI.

Kiitikio: Tumepewa amri tupendane wote,vile Yesu alivyotupenda.

1. Ningesema luga zote,kujua elimu zote, ni bure pasipo mapendo.
2. Ningekuwa na kipaji ya kuagua yajao, ni bure pasipo mapendo.
3. Ningekuwa na imani ya kuhamisha milima, ni bure pasipo mapendo.
4. Hata nikipana mali na vitu kwa wamaskini,ni bure pasipo mapendo.

(Kuimba kiitikio)

5. Mapendo ya vumilia hayajui hata wivu,hayajui kujivuna,
   Mapendo ni makubwa.
6. Hayatafuti faida wala hayakasiriki,na kutakia mabaya,
   Mapendo ni makubwa.
7. Katika vipaji vyote,katika elimu zote za dunia na za mbingu.
   Mapendo ni makubwa.
8. Kuliko Imani yote,kuliko kitumaini,kuliko fazila zote,
   Mapendo ni makubwa.

( Kuimba kiitikio)

## KIAPO CHA UBATIZO

1. Kiapo cha Ubatizo wangu,kutoa simimi,ni wao,ni mzima,nayo akili yangu,ninaapa mwenyewe leo: Ninaapa,ninaapa,ninaapa mwenyewe leo,ninaapa mwenyewe leo.
2. Naapa: Yesu ndiye Mwokozi,sadaka mlipa letu deni,mwenyewe Mwana wa Mwenyezi,naapa ni yangu imani.
3. Naapa;kwa Mungu na Kanisa ni mtoto tangu Ubatizo,ya jana nayatubu makosa: naapa:ni mtu mpya si mchezo.

## ALLELUIA BWANA AMEFUFUKA.

Kiitikio: Utukufu wake kwa milele,mbinguni juu pamoja na Baba.

1. Tumjongelee Yesu mtukufu: Alleluia Bwana amefufuka.
   Amefufuka katika wafu : Alleluia Bwana amefufuka.
2. Mmèona nini ku kaburi, Wewe Magdalena na Salome.
3. Siku tatu kiisha kufa kwake,ametoka peke kaburini.
4. Sasa akuja kwa kutulisha: Mwili wake chakula cha roho.
5. Tukila mwili wake mtukufu: Tutapokea uzima mpya.
6. Mababu wenu wakala mana: Ila njiani wote wakafa.
7. Ila alaaye mwili wangu: Nitampa uzima wa milele.

## EE VIUMBE KARIBUNI.

Kiitikio: Ndiyo sakramenti kuu mwili damu ya Yesu.

1. Ee viumbe karibuni,Mungu wenu kamsifuni.
2. Ee Mariamu utaanza,kumwimbia wew wa kwanza.
3. Nanyi Malaika wote,wa mbinguni mtaitika.
4. Manabii na Mababu,muone jambo la ajabu.
5. Nye Mitume na Wenjili,tukuzeni fumbo ili.
6. Mashaidi waungama,jongeeni kutezama.
7. Nyinyi Mabikira pia,sichokeni kumwimbia.
8. Ee Watakatifu wote,mwimbee nasi siku zote.

## DAMU TAKATIFU.

Kiitikio: Damuni mwako,Wokovu wetu.

1. Mwanzo wa mateso bustani ni Gestemani.
2. Rohoni uchungu,jasho la damu mwilini.
3. Malipo ya Yuda yakawa bei ya damu kuu.
4. Damu takatifu ya mwana kondoo wa Mungu.
5. Sherti imwagike tupisi heri ya mbingu.
6. Miiba ya taji imepakwa damu.
7. Oh ! Oh ! mijeledi na misumari na mikuki.
8. Vidonda vitano,alama ya mapendo tu.
9. Salamu ee Yesu sadaka msalabani.
10. Yesu mkombozi aksanti sana twakupa.

## MKRISTU MIYE.

Kiitikio: Mkristu miye niko salama,shetani we sinijie,si mtumwao
sirudi nyuma,mkristu miye,mkristu miye.

1. Mkristu miye Baba ni Mungu,amri zake nitashika,nitakaa na cheo changu,nipate mimi okoka.
2. Mkristu miye Yesu ni ndugu,siku zote nitampenda,kwani ndiye Mkombozi wangu,kwake nimetaka kwenda.
3. Mkristu miye;Na Mama yangu,nataka kumsikiliza,ndiyo kanisa lake Mungu,ndiyo yenyi kunifunza.
4. Mkristu miye,si wa dunia,nimekataa mamboye,Mungu tu nitamwelekea: Kwani mtoto wako miye.
5. Na alama ya Ubatizo,ya asili zambi sina,yamekwisha na maapizo ya kanisa nili mwana.
6. Ni msafiri wa hapa chini ukomo juu kwa Mungu nafuliza mbio

Archivio Salesiano Roma

## HAKUNA KITU

1. Hakuna kitu kinaweza kututenga na mapendo ya Yesu.
   Hakuna kitu kinaweza kututenga na mapendo ya Yesu.
2. Wala mateso hayawezi kututenga mbali na Mungu.
3. Wala taabu haiwezi " " " "
4. Kufukuzwa hakuwezi " " " "
5. Wala njaa haiwezi " " " "
6. Kuchukiwa hakuwezi " " " "
7. Wala utupu hauwezi " " " "
8. Wala hatari haiwezi " " " "
9. Wala upanga hauwezi " " " "
10. Umaskini hauwezi " " " "
11. Sababu yako tunaishinda masumbuko yetu yote.
    Sababu yako tunaishinda masumbuko yetu yote.
12. Tukivumilia tunaweza kuwa wote sawa kondoo.
13. Mwisho wetu tutafurahiwa pamoja na Bwana Yesu.
    Mwisho wetu tutafurahiwa pamoja na Bwana Yesu.
14. Hakuna kitu kinaweza kututenga mbali na Mungu.
    Hakuna kitu kinaweza kututenga mbali na Mungu.

## TUMSIFU BWANA WETU.

Kiitikio: Tumsifu Bwana wetu Yesu Kristu, katika hostia hii takatifu.

1. Tumwabudu tumsifu Mungu wetu Katika hostia hii takatifu.
2. Alitoa mwili wake mtakatifu " " " "
3. Alitoa damu yake takatifu " " " "
4. Mwili wake ni mkate wa uzima " " " "
5. Ni mkate wa uzima wa milele " " " "
6. Ye mwenyewe akasema kwa Mitume " " " "
7. Aulaye mwili wangu hatapotea " " " "

Archivio Saveriano Roma

8. Ainywaye damu yangu atatakaswa    Katika hostia hii takatifu.
9. Twende basi ee wandugu kwake Yesu    "    "    "    "
10. Tumsifu Bwana wetu Yesu Kristu katika hostia hii takatifu.

## TUMWIMBIE MUUMBAJI.

Kiitikio: Twimbe eeee, Tumwimbie Bwana Mungu wa milele, we wa milele,vyumbe vyako vyote vyasifu kokote ukubwa wako.

1. Tumwimbie Mûmbaji wa mbingu na wa dunia/ Tumtuze na tusifu kwa nyimbo na mayowe. Ndiye peke Mungu Baba Mwenyezi.
2. Tumsifu Bwana Mungu hekaluni pake/Msifuni nanyi anga za mawazo yake,ndiye............
3. Tumsifu matendoye yasiyo na mipaka/Tusifu cheo chake kisicho na kipimo,ndiye........
4. Tumsifu Mwenyezi kwa miziki yetu/ Tumtuze mwumbaji kwa mlio wa vinanda,ndiye.......
5. Tumsifu Bwana Mungu kwa zeze na gitari/ Tumsifu Mwenyezi kwa mpigo wa ngoma,Ndiye...
6. Nanyi ndege,nyama,mumsifu Bwana/ Pepo pia zaruba mtukuze Mwenyezi,Ndiye........

## TUMFUATE TUMKARIBIE.

Kiitikio: Tumfuate,tumkaribie,siku zote na popote (bis)
Yesu mbele,Yesu mbele,Yesu mbele sisi nyuma yake Bwana(bis)

1. Yesu alisema,ombeni mutapewa,chochote muombacho kwa jina langu,mutapewa.
2. Yesu alisema,mimi nipo njia,uzima wa kweli,wakufika kuko Baba,wa mbinguni.
3. Yesu alisema,heri nyinyi wote,wenyi kusema na kuteswa kwa jina langu,mtatulizwa.
4. Yesu alisema,njooni wote kwangu,mimi nipo mwema na mpole,

Archivio Saveriano Roma

5. Mungu alisema,Mwanangu mfungulie,yeyote apigae hodi,
Kwa jina langu,mfungulie.

## ALLELUIA.

Kiitikio: Alleluia,alleluia,alleluia.

1. Msifuni Mungu katika,patakatifu pake.
2. Msifuni Mungu katika,anga la uwezo wake.
3. Msifuni Kwa matendo yake makubwa.
4. Msifuni kwa kadiri ya wingi wa ukuu wake.
5. Msifuni kwa sauti ya baragumu.
6. Msifuni kwa kinanda na kinubi.
7. Msifuni kwa ngoma na michezo.
8. Msifuni kwa zeze na filimbi.
9. Msifuni kwa matoasi yaliyao.
10. Msifuni kwa matoasi yavumayo sana.
11. Kila mwenyi pumzi asifu Bwana.

## ALLELUIA MSIFUNI BWANA.

Kiitikio: Alleluia,alleluia,alleluia.

1. Msifuni Bwana pahali pake patakatifu/Msifuni katika anga la uwezo wake.
2. Msifuni juu ya matendo yake makubwa/ Msifuni juu ya ukubwa wake usio na ukadiri.
3. Msifuni na tarumpeta ya sauti kubwa/Msifuni na kinanda na kinubi.
4. Msifuni na kigoma na ngoma/Msifuni na zeze na kinanda.
5. Msifuni na matoasi yanayolia nguvu/ Msifuni na masahani ya shaba yanayopiga shangwe.
6. Sifa kwa Baba na kwa Mwana/Na kwa Roho Mtakatifu.
7. Kama ilivyokuwa mwanzo na sasa na siku zote/ Na miaka ya milele Amen.

## BABA YETU.

Kiitikio: Tunakusifu, weye Bwana, pokea sala zetu.

1. Baba yetu wa mbinguni
2. Jina lako lisifiwe
3. Ufalme wako uje
4. Mapenzi yako yafanyiwe
   - -Utupe chakula chetu
   - -Makosa yetu samehe
   - -Tukasamehe wenzetu
   - -Tuepushe kishawishi
5. Leo kesho na milele.

Tunakusifu weye Bwana pokea sala zetu.

Pokea sala zetu.

## ALLELUIA, ALLELUIA.

Kiitikio, Alleluia, alleluia, alleluia, alleluia, alleluia.

1. Neno lako we Bwana/ Ni neno la uzima wa milele.
2. Msalaba wako we Bwana/ Utatuletea wokovu wako.
3. Bakia nasi we Bwana/ Tutapata furaha ya milele.

## YESU MPOLE NA MNYENYEKEVU.

Kiitikio: Yesu mpole na mnyenyekevu, uifanye mioyo yetu ifanane na moyo wako.

1. Roho ya Kristu unitakase/ Mwili wa Kristu uniopoe.
2. Damu ya Kristu, uninyweshe/ Maji ya ubavuni mwa Kristu unisafishe.
3. Mateso ya Kristu unitilie nguvu/ Yesu mwema unisikilize.
4. Unifiche katika vidonda vyako/ Usiniache kutengwa nawe.
5. Unikinge na adui yangu mbaya/ Uniite wakati wa kufa kwangu.
6. Uniweke karibu nawe/ Nikusifu pamoja na watakatifu wako/ kwa myaka ya milele. Amen.

## MUNGU NI MLINZI WA WAAMINI.

Kiitikio: Wewe ndiyo kimbilio langu na msaada wangu/ Mungu wangu ninayemwamini.

1. Ukaaye katika ulinzi wake aliye juu/ Ukawiaye kivulini mwa Mwenyezi.
2. Umwambie Bwana: Wewe kimbilio langu na ngome yangu/ Mungu wangu ninayemwamini.
3. Maana yeye atakuponya mkononi mwa mwindaji/ Na katika tauni ya uharibifu.
4. Kwa manyoya yake atakufunika,na chini ya mabawa yake utakimbilia,uaminifu wake ni ngao na kingo.
5. Hutaogopa kitisho cha usiku/Wala mshale urukao mchana.
6. Wala tauni inayotembea gizani/Wala ambukizo linalouwa jua kali.
7. Wanapoanguka watu elfu karibu yako,na elfu kumi mkono wako wa kuume/ Kwa wewe halitafika kamwe.
8. Ila utatazama tu kwa macho yako/ Nawe utaona malipo ya waovu.
9. Kwa maana kimbilio lako ni Bwana/ Umemchagua aliye juu kuwa ngome yako.
10. Tukio mbaya halitafika kwako/Wala maangamizo yatakaribia hema yako.
11. Maana amekuagizia malaika wake/wakulinde katika njia zako zote.
12. Mikononi mwao watakuchukua/ Usijikwae mguu wako jiweni.
13. Utakwenda juu ya pili na mamba/ Utakanyaga mwana simba na nyoka.
14. Kwa kuwa ameambatana nami/ Nitamwokoa nitamlinda kwa kuwa amejua jina langu.
15. Ataniomba nami nitamsikiliza,nitakuwa naye katika taabu/ ni mwokoa na kumpa heshima.
16. Nitamshibusha kwa wingi wa siku/ Nami nitamwonyesha wokovu wangu.

Archivio Saveriano Roma

## AKSANTI BWANA.

Kiitikio: Aksanti Bwana twapiga aksanti, unayeishi milele na milele.

1. Kwa maisha yetu nzima.
2. Kwa mapendo yako makuu.
3. Kwa wokovu wako kamili.
4. Kwa maondoleo ya zambi.
5. Kwa uzima wetu wa Roho.
6. Kwa uzima wetua wa milele.

## NITAJONGEA ALTARE YA MUNGU.

Kiitikio: Nitajongea altare ya Mungu furaha ya vijana.

1. Iwe tu sawa mbele yangu/ Niopoe kwa ubaya wote.
2. Sababu ndiwe Mungu wangu/ Kwani ninaona uchungu.
3. Peleka mwanga na amani/ Viniongoze juu kwako.
4. Nami nitajongea e Mungu/ Na Roho safi na mapendo.
5. Nami nitakuimbia ee Mungu/ Salama na furaha zetu.
6. Sifa kwa Baba/ na Mwanae/ Na Roho mtakatifu.

## MAMA MARIA MAMA.

Kiitikio: Mama Maria mama, utufungulie (bis) Sisi wana wako mama tunapiga hodi(bis).

1. Munataka nini/enyi wana wangu(bis)
   tunataka kumwona mtoto wako Yesu (bis).
2. Enyi wana wangu, mukaeni hapa (bis)
   Ninaenda kumwita mtoto wangu Yesu (bis).
3. Mukiona Yesu, musipate woga (bis).
   Yeye ana mwili kweli wa kuleta woga (bis).

4. Ee Yesu wangu,uje kuona (bis)
Wale wajamaa letu la mu duniani (bis).
5. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho (bis)
Kama mwanzo na daima na milele Amen (bis).

## AVE MARIA YOO MARIA.

Kiitikio: Ave Maria yoo Maria,ave ave Maria ee.

1. Mama Maria mpenzi wetu,ulifika kwa Bernadetta.
2. Mama Maria humu mu Zaïre ifanyike sawa ku Lourdes.
3. Hata mu furaha hata mu mateso tuwe nawe Maria ee.
4. Wewe ndiyo mama,hakuna mwengine mama mwema Maria ee,
5. Mama Maria umejaliwa neema,kuliko wanawake wote.
6. Baba wa mbingu,amekubariki,tangu mwanzo Maria ee.
7. Mlango wa m'bingu,mwanga wa dunia,tuongoze Maria ee.

## MAMA MARIA MPOLE.

Kiitikio: Mama Maria mpole,Bikira Maria mpole,hatuna chochote cha kukutolea,Mama Maria mpole,Pokea mawazo na sala zetu, mama Maria mpole.

1. Mama Maria mpole,bikira Maria mpole,tunakuita leo utusikilize, mama Maria mpole. Utusaidie ayo tuombayo,mama Maria mpole.
2. Mama Maria mpole,mulango wa mbingu mpole,tunakumbuka mateso yako,mama Maria mpole,siku ulikuwa chini ya msalaba,mama Maria mpole.
3. Mama Maria mpole,mama wa muumba mpole,tunakutolea mateso yetu, Mama Maria mpole,sisi wa vipofu wa bin'adamu,MamamMaria mpole.
4. Mama Maria mpole,mama wa muumba mpole,tunakutolea mateso yetu Mama Maria mpole,tunakutolea dunia yote;Mama Maria mpole.

## E BIKIRA MWEZAJI.

Kiitikio: Ave Maria,Tafazali nifazili,na uzima e Mama Mwema
Ave,ave,ave Maria.

1. Ee Bikira mwezaji,ave Maria,Musikilize mwombaji ave Maria.
2. Dunia ni daima, zaruba zinavuma.
3. Wa utoto zaifu,ukingie unyofu.
4. Ulinde wa ujana,uzuri na heshima.
5. Uwe mfariji wao,wazee watupwao.
6. Tazamia makao,ya wenye wateswao.
7. Wemao upendezi,wakomesha machozi.
8. Wawiye dawa bora,walio na ugonjwa.
9. Mama ukae nasi,kufuga moyo mwasi.

## EEE MARIA MAMA MZURI.

1. Ee Maria mama mzuri,ukumbuke ukaone,wengi wa watoto wako wanaoteswa toharani.
2. Kwa uwema wako mama,uwahurumie wale,wanaosumbuliwa sana moto ukiwaangamiza.
3. Kwako mama tunaomba ukumbuke kwetu pia,tusiteswe na tamaa,tufike kule mbinguni juu.

## BIKIRA WA SIFA - Alma redemtoris Mater.

Kiitikio: Bikira wa sifa salamu mama Maria.

1. E mama mzazi wa mkombozi,we uliye mlango wa uwingu,Daima wazi salamu.
2. We nyota safi ya bahari,uwasaidie waangukao,wanaotaka kuamka.
3. Dunia yote inakusangaa,kwani umemzaa Mwanao,muumba wako mtukufu.
4. We ni Bikira mbele ya kuzaa,wabaki bikira kiisha kuzaa,mzao bora Kristu.

Archivio Salesiano Roma

5. Pokea basi maamkio yetu,kama yale aliyokutolea,Gabrieli malaika.
6. Tunakuomba uwahurumie,wenyi zambi masikini,We Bikira huruma.

## AVE MARIA.

Kiitikio: Ave Maria,Mama angu salamu,nakusalimu,ave Maria.
1. Juu malaika makundi heri,sifazo witika kwa wimbo mzuri.
2. Twakushangilia,nasi wanao,heshima pokea kwetu wajao.
3. Mnyonge kwako Mama hutumaini;mwokoe salama mtie auni.
4. Kumbuka msalaba wa Mwana mpenzi,waja wakuomba ndiwe mwombezi.

## LITANIA YA BIKIRA MARIA.

| WAIMBAJI | | | WOTE | |
|---|---|---|---|---|
| Tumshangilie | | Bikira Maria | Tumshangilie | Bikira Maria (bis). |
| 2. | " | Mama mtakatifu | " | Mama mtakatifu |
| 3. | " | Mama wa neema | " | Mama wa neema |
| 4. | " | Mama bila zambi | " | Mama bila zambi |
| 5. | " | Mama bila taka | " | Mama bila taka. |
| 6. | " | Mama mpendelevu | " | Mama mpendelevu. |
| 7. | " | Mama wa muumba | " | Mama wa muumba. |
| 8. | " | Mama wa Mwokozi | " | Mama wa Mwokozi |
| 9. | " | Bikira wa sifa | " | Bikira wa sifa |
| 10. | " | Bikira Mwezaji | " | Bikira Mwezaji. |
| 11. | " | Bikira wa huruma | " | Bikira wa huruma. |
| 12. | " | Chombo cha neema | " | Chombo cha neema. |
| 13. | " | Chombo cha hekima | " | Chombo cha hekima. |
| 14. | " | Mnara wa Daudi | " | Mnara wa Daudi. |
| 15. | " | Mnara wa pembe | " | Mnara wa pembe. |
| 16. | " | Nyumba ya zahabu | " | Nyumba ya zahabu. |
| 17. | " | Mlango wa mbinguni | " | Mlango wa mbinguni. |

18. Tumshangilie Nyota ya asubui: Tumshangilie nyota ya asubui.
19. " Afia ya wagonjwa " Afia ya wagonjwa.
20. " Malkia wa mitume " Malkia wa mitume.
2I. " Malkia wa amani " Malkia wa amani.

## LITANIA YA BIKIRA MARIA.

Bwana,utuhurumie.
Kristu,utuhurumie.
Bwana,utuhurumie.
Kristu, utusikie.

Baba wa mbinguni,Mungu, utuhurumie.
Mwana Mkombozi wa dunia,Mungu,utuhurumie.
Roho Mtakatifu Mungu,utuhurumie
Utatu Mtakatifu,Mungu mmoja,utuhumie.
Maria mtakatifu,utuombee.
Mzazi mtakatifu wa Mungu,utuombee.
Bikira mtakatifu wa mabikira , Utuombee.
Mama wa Kristu
Mama wa neema ya Mungu,
Mama asiyejua zambi,
Mama wa moyo safi,
Mama mwenyi ubikira,
Mama usiye na taka,
Mama mpendelevu,
Mama mzuri sana,
Mama wa shauri ngema,
Mama wa Muumba,
Mama wa mkombozi
Bikira mwenyi utartibu,
Bikira mwenyi heshima,

Bikira wa sifa, utuombee
Bikira mwezaji,
Bikira mwenyi huruma
Bikira amini,
Kioo cha haki,
Kikao cha hekima,
Sababu ya furaha yetu,
Chombo cha meema,
Chombo cha hekima,
Chombo bora cha ibada,
Waridi uliofumbwa,
Mnara wa Davidi,
Mnara wa pembe,
Nyumba ya zahabu,
Sanduku la maagano,
Mlango wa mbingu,
Nyota ya asubui,
Afya ya wagonjwa,
Makimbilio ya wakosefu,
Mtuliza wa wenyi uchungu,
Msaada wa wakristu,
Malkia wa Malaika,
Malkia wa mababu,
Malkia wa manabii,
Malkia wa mitume,
Malkia wa mashaidi,
Malkia wa waungama,
Malkia wa mabikira,
Malkia wa watakatifu wote,
Malkia uliyeumbwa pasipo kosa la asili,
Malkia uliyepokewa mbinguni,
Malkia wa rozario takatifu,
Malkia wa amani.

Archivio Saveriano Roma

Mwana-kondoo wa Mungu unayeondoa zambi ya dunia,utuondolee,Bwana,
Mwana-kondoo wa Mungu unayeondoa zambi ya dunia,utusikilize,Bwana.
Mwana-kondoo wa Mungu unayeondoa zambi ya dunia,utuhurumie.

## KWA KUMSIFU MUNGU.

1. Mungu atukuzwe/ Litukuzwe jina lake takatifu.
2. Atukuzwe Yesu Kristu/ Mungu kweli na mtu kweli.
3. Litukuzwe jina la Yesu/ Utukuzwe moyo wake mtakatifu.
4. Atukuzwe Yesu/ Katika Sakramenta kuu ya altare.
5. Atukuzwe Mama mtukufu wa Mungu/ Bikira Maria mtakatifu.
6. Atukuzwe Maria mtakatifu/ Aliyeking zambi ya asili.
7. Litukuzwe jina la Maria/ Bikira na mama.
8. Atukuzwe Yusufu mtakatifu/ mume wake wa usafi bora.
9. Atukuzwe Mungu katika malaika/ Na watakatifu wake.
10. Atukuzwe Maria mtakatifu,aliyepalizwa mbinguni.

## ONJENI

Kiitikio: Onjeni na angalieni namna gani Bwana alivyo mwema,heri mwenyi ku kimbilia kwake.

1. Nitamtukuza Bwana kila wakati,sifa yake kinwani mwangu daima.
2. Roho yangu ijisifu katika Bwana,wanyonge wasikie na kufurahi.
3. Mtukuzeni Bwana pamoja nami,tukuzeni jina lake wote pamoja.
4. Nalimkimbilia Bwana akanisikiliza,akani[illegible]poa katika hofu yangu yote.
5. Mnyonge huyu alilia na Bwana akamsikiliza akamwokoa katika shida zake zote.
6. Onjeni mukaone ginsi Bwana alivyo mwema,heri mtu yule anaye-mkimbilia.
7. Mcheni Bwana enyi watakatifu wote,kwa maana wenyi kumcha hawakosi kitu.

8. Njooni waana munisikie/ Nitawafundisha uchaji wa Bwana.
9. Nani mtu apendaye uzima/ Anayetaka kuona heri.
10. Zuilia ulimi wako mbaya/ na midomo yako isiseme udanganyifu.
11. Uepuke na ubaya utende mema/ tafuta amani ukaifuate.
12. Macho ya Bwana yaangalia wanyofu/ Na masikio yake yaelekea mlio wao.
13. Uso wa Bwana wawageukia watenda mabaya/ Ili aongoe kumbukumbu lao duniani.
14. Wanyonge wameita na Bwana awasikiliza/ awaopoa katika taabu zao zote.
15. Bwana ni karibu na waliopondeka moyo/ awaopoa wenyi kuvunjika roho.
16. Mateso ya mnyofu ni mengi/ lakini Bwana amwokoa katika yote.
17. Alinda mifupa yake yote/ Hata moja yao hautavunjika.
18. Ubaya unamwuwa mwovu/ nao wenyi kumchukia mnyofu wataazibiwa.
19. Bwana anakomboa roho za watumishi wake/ wote waliomkimbilia hawataazibiwa hata.

## TUMSIFU MARYAMU.

Kiitikio: Ave,ave,ave Maria,ave,ave,ave Maria.

1. Tumsifu Maryamu,enyi wanae,tutoe salamu,tumshangilie.
2. Katika uwingu ni mfalme mkuu,nyuma yake Mwanga wa kwanza juu.
3. Nyota ya bahari,mlango wa mbingu;mwondoa hatari,mama wa Mungu.
4. Maryamu Bikira,ndiye mteule,ndiye mwana bora tangu milele.
5. Ameitwa mfalme wa malaika,mfalme wa mitume,mkanyaga nyoka.
6. Hatuna mwombezi atuombee kwa Mungu,mwenyezi kuliko yeye.

Archivio Saveriano Roma

## MAMA MARIA JAMBO.

Kiitikio: Mama Maria jambo/ Maria wa Mwokozi jambo
Mama hatuna kitu cha kukupa mama: Mama Maria wetu jambo
Mama nyoyo zetu zote zajaa na zambi: zambi mama Maria
wetu jambo.

1. Ee mama (2x) Mama Maria wetu mama Maria wetu jambo.
E mama wa Mwokozi "
Tuunganishe na mwanako "
Tuwe naye mu dunia "

2. Ee mama (2x) Maria utupe Yesu "
Yesu utupe Maria "
Ulimwacha kwa Yoani "
Ndiyo kwetu sisi wote "

3. Ee mama (2x) Dunia hatuna kitu "
Masumbuko na mateso "
Tumfuate mu mbinguni "
Tufurahiwe milele "

4. Ee mama (2x) Uje utubarikie "
Fukuze shetani mbali "
Nyoyo zetu ni regevu "
Kaa kwetu usitoke "

5. Ee mama (2x) Wivu chuki na hasira "
Unafiki na uvivu "
Ongeza uzazi kwetu "
Ututie uzima "

6. Ee mama (2x) Utugawie mapendo "
tuonyeshe Mwana wako "
Mu mawazo yote tatu "

7. Ee mama (2x) Sifa kwako Mungu Baba,mama Maria wetu jambo.
Sifa kwako Mkombozi "
Naye Roho Mtakatifu "

## EE BWANA YESU.

Kiitikio: Ee Bwana Yesu,we mwokozi,katika hostia unakaa kweli
Ufike leo,ulishe yetu roho,tukupende,tukubarikie
Yesu mwema.

1. Ee Yesu mfazili,utupe imani tuzidi kusadiki mafumbo yako.
2. " " " mapendo tuzidi kuungana na moyo wako.
3. " " " Imara tuzidi kuifwata sheria yako.

## MWENYEZI AMEKUJA NEEMA.

Kiitikio: Mwenyezi amekujaza neema,neema nyingi sana,salamu we
Mamae.

1. Sikia mwanangu natega sikio,sahahu nyumba na ukoo wa Baba yako.
2. Hivi mfalme atatamani uzuri wako,kwani ni Bwana wako ukamweshimu.
3. Binti wa Tyro atakufurahisha,atakufurahisha na zawadi zake.
4. Na mataifa tajiri hupita yote,yatakuletea mavazi mengi yenyi zaabu.
5. Binti wa mfalme akivaa vazi lenyi zaabu,anapelekwa nyumbani kwa mfalme.
6. Na wabinti rafiki zake wamfuata,wanaingizwa nyumbani kwa shangwe kubwa.
7. Watakuwa wanao pahali pa baba zako,utawakuza katika inchi zote.
8. Nitalikumbusha jina lako kwa vizazi na vizazi,ili mataifa yakusifu milele.
9. Asifiwe Baba na Mwana na Roho mtakatifu,kama mwanzo na sasa na milele Amen.

Archivio Saveriano Roma

## WIMBO WA MSALABA MTAKATIFU.

Kiitikio: Ee Bwana tunaabudu,msalaba wako mtukufu,tunatukuza na tunasifu ufufuo wako mtukufu.

1. Tumwimbie Kristu Bwana,aliyepigana kwa sifa,kwa msalaba wake alishinda zambi na kufa,Tumwimbie Mkombozi wetu kwa kufa kwake alishinda.
2. Bab'Adamu aliasi,na kwa kula tunda la mti akafa,katufisha si wanae sababu ya zambi. Lakini Mungu Baba yetu akahurumia maskini.
3. Wakati ulipofika,Mwana wa Mungu katujia,Betlehemu akazaliwa: Mamae Maria,Tumboni mwake katwâa mwili,akajifanya mtu kweli.
4. Na pa kuzaliwa kwake horini nyasini kalazwa,Bikira Maria Mamae Akamtunza,akamvika,akamtuliza,Mwanae alipolia.
5. Pa myaka makumi tatu,wakati wa ukatimia,Mwokozi kakubali kuteswa, Kwa mapenziye,Msalabani akapanda,Atolee sadaka bora.
6. Miiba,mkuki,misumari,Vikapenya msalabani,Ubavuni yakatiririka Maji na damu,Kwa huu dunia na mbingu,Na watu wote wameoshwa.
7. Ee muti mtakatifu,Mwenyi wekundu wa damu,Damu yake Yesu Kristu Mungu ulichukua,ukawa altare ya sadaka inayokomboa wazambi.
8. E msalaba,twakuabudu tukuonapo twamkumbuka,Yesu Kristu Mkombozi wetu,Twamshukuru:Kwa mateso na kufa kwake,Pendo kubwa ameonya.
9. Kwako sifa ya milele,E Utatu Mtakatifu,Sifa moja Baba na Mwana Na Roho mtukufu,Dunia,sifu nafsi tatu,Katika Mungu mmoja, Amen.

## NJIA YA MSALABA.

1. BWANA YESU MPENDELEVU -- huruma
anahukumiwa afe -- huruma
kwa ajili ya wazambi -- huruma
akiteswa msalabani -- huruma

2. Bwana Yesu mpendelevu
alijitwika msalaba
akaanza kuingia
kwa safari ya Kalvario

3. Bwana Yesu mpendelevu
anaanguka mpaka chini
akishindwa na uzito
wa msalaba na wa zambi

4. Bwana Yesu mpendelevu
anamkuta mama yake
akilia na machozi
ya uchungu kubwa mno

5. Bwana Yesu mpendelevu
asaidiwa na Simoni
kwa sababu nguvu zake
zinaanza kuregea

6. Bwana Yesu mpendelevu
uso wake mtakatifu
wenyi jasho wenyi damu
apangusa Veronika

7. Bwana Yesu mpendelevu
anaanguka mara pili
wanataka kumlilia
na naye anawatuliza

8. Bwana Yesu mpendelevu
wanawake kwa huruma
wanataka kumlilia
naye anawatuliza

9. Bwana Yesu mpendelevu
anaanguka mara tatu
kwani sasa anachcka
anataka hata kufa

10. Bwana Yesu mpendelevu
ananyanganyiwa nguo
yeye mwenyi anavika
vyumbe vyote vya dunia

11. Bwana Yesu mpendelevu
anapigwa misumari
anawekwa msalabani
watu wanamchekelea

12. Bwana Yesu mpendelevu
anakufa msalatani
roho yake yazimia
na sadaka yatimia

13. Bwana Yesu mpendelevu
anashushwa msalabani
Na Mamae Mtakatifu
mikononi anampokea

14. Bwana Yesu mpendelevu
anazikwa kaburini
Sisi wote tumlilie
ndivyo Yesu ametupenda.

++++++++++++++++++++++

Archivio Saveriani Roma

## TUNAKUSALIMU BIKIRA MARIA

1. Tunakusalimu, tunakusalimu Bikira Maria aaa
Mama wa Bwana wetu, mama wa Bwana wetu Bikira Maria aaa
Malkia wa mbinguni, malkia wa mbinguni Bikira Maria aaa

2. Afrika ni yako, Afrika ni yako Bikira Maria aaa
Tunakupenda sana, tunakupenda sana Bikira Maria aaa
Wee mama wetu mwema, wee mama wetu mwema Bikira Maria aaa

3. Utusaidie, Utusaidie Bikira Maria aaa
Takasa nyoyo zetu, takasa nyoyo zetu Bikira Maria aaa
Pandisha Roho zetu, pandisha roho zetu Bikira Maria aaa

4. Fukuza shetani, fukuza shetani Bikira Maria aaa
Tukingie hatari, tukingie hatari Bikira Maria aaa
Ulinde wana wako, ulinde wana wako Bikira Maria aaa

5. Mama wa Mitume, mama wa mitume Bikira Maria aaa
Tuvute watu wengi, tuvute watu wengi Bikira Maria aaa
Wawe watoto wako, wawe watoto wako Bikira Maria aaa.

## MARYAMU BIKIRA, TUMSHANGILIE

Kiitikio: Tumsifu, tumsifu, tumsifu Maryamu, Tumsifu, tumsifu, tumsifu maryamu.

1. Maryamu bikira tumshangilie, Mama wetu mwema tumkimbilie.
2. Pasipo kilema tangu asili; waitunza nzima hiyo fazili.
3. Kumwona Jibrili wafazaika, nenole kubali tutaokoka.
4. Wakushangilie humu wizazi, kwani wamfumbia wao Mkombozi.
5. Wa Mwanae Mungu u Mama mzazi; muumba uwingu ndako msikizi.

## SALAMU MALIKIA WA MBINGU.

kiitikio: Salamu,salamu malkia wa mbingu;
We mama wa Mwenyezi salamu.

1. Salamu,weye mkubwa wa Malaika,salamu shina,salamu,mlango,salamu.
2. Ndiwe,uliye leta mwanga duniani,furahi sana Bikira mtukufu,salamu.
3. Upo mzuri kupita wote salamu Mama,weye mpambe,tuombee Kristu salamu.

## TWAKUSALIMIA.

1. Twakusalimia,e Maryamu
Twakuangukia,e Maryamu
E Maryamu,shime,
Mama situnyime.

2. Ndisi wana wako,e Maryamu.
Twakuomba sana, e Maryamu.

3. Usituchukie, e Maryamu.
Utufanyizie, e Maryamu.

4. Twakutumaini,e Maryamu.
Hapa ugenini,e Maryamu.

5. Ndiwe wetu mjima,e Maryamu
Utujie hima, e Maryamu.

6. Tuombee mema, e Maryamu.
E Bikira mwema,e Maryamu.

7. Hasa tukumbuke,e Maryamu.
Zambi tuepuke, e Maryamu.

8. Moyo tutakate, e Maryamu.
Neema tuipate, e Maryamu.

9. Mwisho tujilie,e Maryamu.
Mbingu tupatie,e Maryamu.

## WE KIMBILIO LETU. Zaburi 89.

Kiitikio: We kimbilio letu toka zamani hizo,zamani za kale.

Archivio Saveriano Roma

1. Mbele milima iweko — We Bwana wetu.
Mbingu na dunia viweko — We Bwana wetu.
Wewe ulikuwa milele — We Bwana wetu.

2. Umewarudisha watu — We Bwana wetu.
Uvumbini kiwambia — We Bwana wetu.
Rudini nyi wanaAdamu — We Bwana wetu.

3. Kwani mbele yako Bwana — We Bwana wetu.
Myaka mia siku moja — We Bwana wetu.
Ipitayo kama maji — We Bwana wetu.

4. Mfano wetu ni maua — We Bwana wetu.
Asubui yachanua — We Bwana wetu.
Mangaribi yakauka — We Bwana wetu.

5. Na hasira yako Bwana — We Bwana wetu.
Ikiwaka juu yetu — We Bwana wetu.
Mara watudidimisha — We Bwana wetu.

6. Makosa yetu wayajua — We Bwana wetu.
Zambi zetu zipo wazi — We Bwana wetu.
Mwanga wako wazi jua — We Bwana wetu.

7. Umri wetu simkubwa — We Bwana wetu.
Saba makumi ao nane — We Bwana wetu.
Ndiyo kinyume cha mateso — We Bwana wetu.

8. Fanya Bwana tuzijue — We Bwana wetu.
Kabisa siku zote — We Bwana wetu.
Hekima bora tupatie — We Bwana wetu.

9. Usijitenge nasi Bwana — We Bwana wetu.
Hima utusimamie — We Bwana wetu.
Watumwa wako hurumie — We Bwana wetu.

100 Huruma yako tujazie
Tufurahi nawe Bwana
Hivyo ime siku zote

We Bwana wetu.
We Bwana wetu.
We Bwana wetu.

## TUFIKE WOTE KWA MISA.

1. Tufike wote kwa misa
watoto wa Mungu (bis)
+ Tufike wote kwa misa
Watoto wa Mungu mwema.

2. Tutubu makosa yetu
sisi wenyi zambi (bis)
+ Tutubu makosa yetu
sisi wenyi zambi nyingi.

3. Tuombe nguvu kwa Mungu
Kwa kazi zetu (bis)
+ Tuombe nguvu kwa Mungu
Kwa kazi zetu za siku.

4. Tusali kwa watu wote
Na inchi yetu (bis)
+ Tusali kwa watu wote
Na inchi yetu Zaïre.

5. Tusali kwa wapagani
Wapende Mungu (bis)
+ Tusali kwa wapagani
wapende Mungu wa kweli.

6. Aksanti sana kwa Mungu
Kwa vitu vyote (bis)
+ Aksanti sana kwa Mungu
Kwa vitu Alivyotupa.

7. Tusali wote pamoja
Tusali vizuri (bis)
+ Tusali wote pamoja
Tusali vizuri sana.

## KWA BIKIRA MARIA.

1. Sisi watoto wako ee Maria,wote twakuangukia huku.
Pokea sifa na shukrani pia,twakutolea mapendo makuu
We Mama wetu Bikira Maria,kwa wema wako tunakusifu,
Ukumbuke twakuomba sana,utulinde na shirika yetu.

Archivio Saveriano Roma

2. We Bikira na Mama wa mapendo,utupeleke kwa Yesu mwema.
   Sisi leo tunakutolea moyo,kwa wema na kwa ulinzi bora.
   Utuombee sana kwa Mwanao,fazila zote zinazotufaa.
   Ndizo upole,usafi wamoyo,mapendo,imara kamili. (2x).
3. Aksanti Mama kwa msaada wako,kwa wema na kwa ulinzi wako bora
   Wote twakuomba ulinde mapendo fazila na naziri za wito.
   Wana wako wakimbilia kwako uwakinge katika hatari.
   Mbinguni tutaimba na Mwanao,huruma na mapendo ya Mama. (2X)

## MAGNIFICAT.

Kiitikio: Nimetendewa mambo makuu,alleluia.
Bwana ni mtakatifu alleluia.

1. Moyo wangu unamsifu Bwana/ Na roho yangu inafurahiwa na Mungu mwokozi wangu.
2. Kwa maana ameungalia udogo wa mtumishi wake/ Tangu leo watu wote watanitaja mwenyi heri.
3. Kwa maana Mwenyezi amenitendea mambo makuu/ Jina lake litukuzwe.
4. Huruma yake inaenea nyakati zote/ Kwa watu wenyi kumfuata sawasawa.
5. Mkono wake umefanya nguvu/ Amewatupilia mbali wenyi kujivuna moyoni.
6. Akawashusha wakubwa katika viti vyao/ Akawapandisha wadogo.
7. Wenyi njaa akawajaza mali/ Na wenyi mali akawafukuza mikono mitupu.
8. Akikumbuka rehema zake/ Amesimamia Israëli mtoto wake.
9. Kama alivyowaambia Ibrahimu/ Na uzao wa siku zote.
10. Sifa kwa Baba na Mwana na Roho mtakatifu/ Kama ilivyokuwa mwanzo na sasa na daima na milele.Amen.

## MOYO WANGU HUMTUKUZA RABI (Magnificat)

Kiitikio: Mwenyezi amenitendea makuu: Jina lake litukuzwe.

1. Moyo wangu humtukuza Rabi,na roho yangu imeshangilia,katika Mungu mwokozi wangu.
2. Kwa kuwa ameungalia,Unyenyekevu wa mtumishi wake,Kumbe tangu toka sasa,vizazi vyote watanitaja mwenyi heri.
3. Kwa maana mwenyezi,amenitendea makuu,na jina lake ni takatifu.
4. Na huruma yake,Ni ya tangu kizazi na kizazi,kwa hao wenyi kumcha.
5. Ameonyesha enzi kwa mkono wake,Amewatawanya,Wenyi kiburi moyoni.
6. Amewashusha,wenyi cheo kikubwa,Akawakuza wanyenyekevu.
7. Wenyi njaa amewashibisha mema,wenyi mali,amewarudisha mikono mitupu.
8. Amempokea Israël,Mtumishi wake,Akiikumbuka huruma yake.
9. Jinsi alivyowaambia baba zetu,Juu ya Ibrahimu,na kizazi chake hata milele.
10. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho;kama mwanzo na daima na milele Amen.

## SALAM BABA

1. Salam Baba wa Mwokozi, Baba,ewe Baba
Salam mlinzi wa Mkombozi, Baba ewe Baba.
Salam Yosef siku hii, Baba,Baba,ewe mlishi baba,ewe,ewe Baba mwema,Ee Bwana wa Maria,utulinde vema.

2. Salam Mume wa Maria, Baba ewe Baba
Mlishi wake Yesu bora " " "
Twakusifu Yosef ee , Baba,baba,ewe mlishi Baba,ewe,ewe Baba mwema ew Bwana wa Maria utulinde vema.

3. Naye Mama kuonana, Baba ewe Baba.
Naye Mwana kupendana " " "
Ndiyo kweli heri kuu, Baba,Baba,ewe Baba,ewe,ewe Baba mwema ee Bwana wa Maria,utulinde vema

4. Uwinguni tuonane , Baba ewe, Baba.
Na milele tupendane, " " "
Tusaidie Yosef ee , Baba,Baba ewe mlishi Baba,ewe,ewe Baba
mwema,ee Bwana wa Maria utulinde vema.

## UJE ROHO MUUMBAJI (Pentekoste.)

1. Uje Roho muumbaji;utazame nyoyo zako;Uzijaze neema nyingi
ulizoziumba nyoyo.
2. Unaitwa mfariji,paji la aliye juu;chemchem ya uzima moto,
pendo na la Roho pako.
3. Wewe mwenyi paji saba;chanda cha kuume Mungu,kiagano we cha
Baba,unazisemesha ndimi.
4. Nia zetu angazia nyoyo jaza na mapendo,mwili wetu mzaifu
ukapate nguvu kwako.
5. Mbali ufukuze pepo na amani tupe hima,hivyo uwe kiongozi,
tuepuke kila zambi.
6. Kwako tukamjue Baba,tena tumtambue Mwana,nawe tunakusadiki
Roho utokaye kwao.
7. Mungu Baba atukuzwe,Mwana aliyefufuka, naye tena mfariji,
Kwa milele na milele.

## NJOO WANGU MFARIJI.

Kiitikio: Njoo wangu Mfariji,yako shusha mapaji,Roho Mungu njoo !

1. Hekima nishushie
Mungu nimfuatie
Roho Mungu njoo !

2. Akili nijalie
Imani nizidie
Roho Mungu njoo !

3. Nieneze shauri
Nishike njia nzuri
Roho Mungu njoo !

4. Nizidishie nguvu
Nisifanye uregevu
Roho Mungu njoo !

5. Elimu nieleze
Hakika niongoze
Roho Mungu njoo !

6. Ibada niwashie
Peke nikuangukie
Roho Mungu njoo !

7. Uchaji nitilie
Zambi nizichukie
Roho Mungu njoo !

## UMTUME ROHO YAKO.

Kiitikio: Roho mtakatifu toka juu.

1. Umtume Roho yako ee Baba wa mbinguni.
2. Umtume Roho yako ee Mwana Yesu Kristu.
3. Ee Roho mtakatifu utushukie hima.
4. Uvumi ukatoka mitume wakamwona.
5. Utupe mwanga wako tuone njia zetu.
6. Utupe kutambua kupendelea mema.
7. Kwa pendo lako wewe uponye majeraha.
8. Utufundishe sisi ukweli wako wote.
9. Safisha Roho zetu kwa nguvu zako wewe.
10. Waweka viongozi kwa kundi lake Yesu.
11. Wajua mabo yote ya Mungu na ya watu.
12. Tuimbe sifa yake tukamtukuze Bwana.

1

## NANI YUPO

1. Nani yupo katika Ukaristia wote: Ni Bwana Yesu.
2. Yupo pale na mwili na damu yake " " "
3. Mzima na mtukufu kama mbinguni " " "
4. Awe chakula cha kulisha roho zetu " " "
5. Ah tunakuabudu wote: E Bwana Yesu.

6. Sisi watoto wako — wote: E Bwana Yesu.
7. Ah tunakushukuru — " " "
8. Kwa ukarimu wako — " " "

9. Mwenyi kutupenda hivi ni nani ? wote: Ni Bwana Yesu.
10. Mwenyi kutupenda hivi ni nani ? " " "

11. Nasi tunakupenda — wote: E Bwana Yesu.

## YESU MWEMA.

Kiitikio: Yesu mwema twakushukuru we.

1. Yesu mwema, we mwabudiwa milele, umetupenda mno.
2. - - unatawala na Baba - -
3. - - ulijifanya mtumishi - -
4. - - ulizaliwa maskini - -
5. - - unastahili mapendo - -
6. - - tumekosea ni kweli - -
7. - - utusamehe na sisi - -
8. - - nasi twapenda mezayo - -
9. - - unatulisha mwilio - -
10. - - unatunywesha damuyo - -
11. - - tusaidie kushinda - -
12. - - ushangiliwe na watu - -

## EE YESU MWEMA KABISA.

1. Ee Yesu mwema kabisa, katika Ukaristia: Nakusadikia.
   Hakika ni Umunguo, mwili roho na damuo: "
2. Ee mfalme wa malaika wa mbingu na wa dunia: Nakutumaini.
   Ee Yesu mwema mwaminini uniweke furahini: "
3. Ee Yesu ninakupenda ulinipenda ya kwanza: Nakupendelea.
   Ufike moyoni mwangu kuondoa uzaifu: "

4. Umwangalie mkosefu, uniambie karibu: Unihurumie.
Ninayatubu makosa, sitakutukana tena "
5. Ufike hima ee Yesu, ufike moyoni mwangu: Uje hima Yesu.
Nakutumaini mfazili, usikawiye rafiki " " "

1. Nakuona na imara umo katika hostia, Nakusadikia.
2. Mimi mtoto masikini, uniopoe zambini, Nakutumaini.
3. Nikiwa na ubaridi, uniwashie moyoni, Nakupendelea.
4. Neema zako uzilete, Yesu unihurumie, Unihurumie.
5. Sema neno moja Bwana, roho yangu itapona, Uje hima Yesu.

## PIGENI MIKONONI Zaburi 46.

Kiitikio: Pigeni pigeni mikoni imbeni kwa furaha, mfalme wa ulimwengu astahili sifa, sifa, ahe mfalme, ahe mfalme, atawale kwetu kote.

1. Enyi wanadamu pigeni mikononi, mshangilie Mungu kwa vilio vya furaha.
2. Kwani Yahwe aliye juu ni mwenyi kitisho, mfalme mkubwa sana wa dunia nzima.
3. Awaweka watu fulani, chini, yetu, na mataifa fulani chini ya miguu yetu.
4. Atuchagulia urisi mzuri, sifa ya Yakobo yeye mpenzi wake.
5. Mungu anapaa katika shangwe kuu, ye Yahwe anapaa katika kelele cha baragumu.
6. Mwimbieni Mungu wetu mwimbeni, mwimbieni mfalme wetu mwimbieni.
7. Yu mfalme wa ulimwengu, mwimbieni kwa moyo wote.
8. Watawalao nchi wafanye makusanyo, pamoja na taifa la Mungu wa Ibrahimu.
9. Wakuu wa dunia ni vyumbe vya Mungu, vya Mungu anayetukuzwa sana milele.
10. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho, kama mwanzo na daima na milele Amen.

## YAHWE AMSIKILIZE Zaburi 19.

Kiitikio: Yahwe amsikilize,Yahwe,Yahwe amfazilie mwenyi aombaye msaada wake.

1. Akwitie Yahwe unapo sumbuka,litukinge jina la Mungu wa Yakobo.
2. Tokea nyumba yake akutume msaada,awe mtegemeo wako tokea Sioni.
3. Ayakumbuke matoleo yako yote,sadaka yako aikubali na mapendo.
4. Akusaidie kadiri ya usafi wa moyo wako,aelekeze vema makusudi yako.
5. Tupige shangwe kwa ajili ya wokovu wako,tuongeze mapambo kwa ajili ya jina la Mungu wetu.
6. Sasa najua ya kwamba Yahwe,atamwokoa mtumwa wake.
7. Toka mbinguni mtakatifu ananijibu,mkono wake wa kuume watupatia wokovu.
8. Fulani waongoza gari,wengine wafuga Farasi,nasi twapenda kuliomba jina la Yahwe Mungu wetu.
9. Hao wavunjika waanguka,nasi twasimama hodari twadumu.
10. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho,kama mwanzo na daima na milele Amen.

## HUZUNI YANGU NI KALI Zaburi 21.

Kiitikio: Huzuni yangu ni kali ee Bwana;usiponitegemea,moyo wangu utaregea hata kuzimia.

1. Nafanana na mkondo wa maji,mifupa yangu yote yaregea.
2. Moyo wangu usawa mta,iyeyukayo kifuani mwangu.
3. Umio wangu hukauka sawa kigaya,ulimi huambatana na kinywa changu;
4. Wamenitoboa mikono na miguu,na kunilaza uvumbini mwa kifo.
5. Nawe kuhesabu mifupa yangu yote,wanaonitazama hunikazia macho.
6. Mavazi yangu wanayagawanya,na joho yangu wanaipigia kura.
7. Ewe Yahwe usikae mbali nami,wewe nguvu yangu unisaidie hima.
8. Ungoe upanga uliopenya moyo wangu,usiiache mbwa kunirarua kwa kucha zake.

9. Uniokoe kinywani mwa simba,Na moyo wangu uepuke na pembe za fahali.
10. Atukuzwe Baba na Mwana,na Roho,Kama mwanzo na daima na milele Amen.

## NANEPA KWA UZITO WA ZAMBI ZANGU Zab. 24.

Kiitikio: Nanepa kwa uzito wa zambi zangu,nishikie mkono Yahwe ee,nisizamie ee maovuni.

1. Bwana ni mwema na mwadilifu,awarudisha njiani bora wapotevu.
2. Wapole waongozwa katika kweli,wanyenyekevu hutembea salama.
3. Njiani pake akuta huruma na haki,anayelinda moyoni ahadi na amri zake.
4. Kwa ajili ya jina lako,unihurumie Bwana,Kwani moyo wangu hujaa vilema.
5. Anayemcha Mungu atambuliwa naye,arudishwa upesi njiani bora.
6. Moyo wake utapangwa herini,na ukoo wake utarisi dunia.
7. Bwana ajifumbulia kwa wamchao,awajulisha agano lake.
8. Atukuzwe Baba na Mwana,na Roho,kama mwanzo na daima na milele Amen.

## FURAHINI EE WANADAMU Zaburi 32.

Kiitikio: Furahini ee wanadamu wenyi moyo mwema: Furahini kwani Yahwe awalinda.

1. Toka mbinguni juu,Yahwe atazama,Awaona vema wanadamu wote.
2. Toka kikao chake awachungulia,wakaaji wote wa dunia.
3. Ndiye aliyeumba moyo wao,na kuzitambua matendo yao yote.
4. Jicho la Yahwe ni kwao wamchao,ni kwao wayangojeao yake mapendo.
5. Yahwe huiponya roho zao kwa kifo,na kuzilishia uzima wakati wa njaa.

Archivio Saveriano Roma

6. Roho yetu hupewa vyote kwa mkono wa Yahwe,Yeye msaada wetu yeye ngao yetu.
7. Moyo wetunhufurahiwa kwake,twalitumainia jina lake takatifu.
8. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho,Kama mwanzo na daima na milele Amen.

## MUNGU WANGU , MUNGU WANGU.

Kiitikio: Mungu,Mungu wangu Mungu wangu,mbona umeniacha.

1. Mungu wangu,Mungu wangu,mbona umeniacha,Mwona umbali na mwito wangu.
2. Ee Mungu wangu nalia mchana kutwa lakini hujibu,nawe wakaa mahali patakatifu.
3. Baba zetu walikutumaini wewe,walikulilia wewe wakaokoka.
4. Lakini mimi nimdudu wala si mtu,wote wanionao wanicheka sana.
5. Wakisema alimtegemea Bwana,Naam,wewe uliyenitoa tumboni.
6. Kwako nalitupwa tangu tumboni,usiwe mbali nami maana ninatabu.
7. Mafahali wengi wamenizunguuka, Wananifumbulia vinywa vyao.
8. Nimemwagika kama maji,moyo wangu umekuwa kama nta.
9. Kaa,kaa langu limekauka kama kigae,umeniweka katika mavumbi ya mauti.
10. Kusanyiko la waovu wamenisonga,naweza kuihesabu mifupa yangu yote.

## WAPANDAO NA MACHOZI Zaburi 125

Kiitikio: Wapandao na machozi wanavuna na furaha.

1. Bwana alipowarudisha wafungwa wa Sion,tulikuwa kama wenyi kuota ndoto,halafu vinywa vyetu vikajaa na cheko,na midomo yetu na nyimbo za furaha.
2. Halafu ikasemeka kwa mataifa,Yahwe aliwatendea makuu,kweli Yahwe alitutendea makuu,tunafurahi.

3. Rudisha Bwana wafungwa wetu,kama mto kujangwa la Negebu,
   wenyi kupanda na machozi wanavuna na furaha.
4. Anatembea na kilio,yule anayechukua mbegu za kupanda,na
   anarudi na kelele ya furaha,akileta mavuno mazuri.
5. Sifa kwa Baba mweza yote,na kwa Mwana mkombozi wetu,na kwa
   Roho mtakatifu akaaye ndani,mwetu: Kama mwanzo na sasa
   na daima na milele  Amen.

## MUNGU NI MCHUNGAJI WANGU?SIKOSEWI KITU

Zaburi: 22

Kiitikio: Mungu ni mchungaji wangu,sikosewi kitu.

1. Mungu ni mchungaji wangu sikosewi kitu,ananiweka kwenyi malisha mazuri.
2. Ananipeleka nipumzike kunako maji,anaipatia roho yangu ujambo
3. Ananiongoza nitembee wima,kwa sifa ya jina lake.
4. Hata nikipita katika bonde linalo magiza,sitaogopa mabaya yote kwani upo nami.
5. Fimbo na bakora yako ya uchungaji zinanituliza,unaniandalia meza mbele ya adui zangu.
6. Unanipaka mafuta kichwani,kikombe changu kinajaa kabisa.
7. Neema na heri yananisindikiza,siku zote za maisha yangu.
8. Nitakaa kwa nyumba ya Bwana,kwa milele na milele.
9. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho mtakatifu,kama ilivyokuwa mwanzo sasa daima na milele  Amen.

## AKSANTI YESU.

Kiitikio: Aksanti Yesu kwa mema yako.

1. Aksanti Yesu kwa mema yako.
2. Tunakuabudu we Mungu wetu.
3. Tunakusifu,unatupenda.

4. Ufike kwangu nikupendeze.
5. Utupe sisi baraka yako.
6. Sisi wakristu,watoto wako.
7. Tunasadiki rehema yako.
8. Na ufanye rehema sana.

## YESU MWEMA.

Kiitikio: Yesu mwema fanyiza kukae ndani mwako nawe ukae ndani mwetu.

1. Musipokula mwili wangu na kunywa damu yangu/ Hamtakuwa na uzima ndani mwenu.
2. Mwenyi kula mwili wangu na kunywa damu yangu ana uzima wa milele,nami nitamfufua siku ya mwisho.
3. Mwili wangu ni chakula kweli na damu yangu ni cha kunywa kweli atakayekula mkate huo atakuwa mzima milele.
4. Mwenyi kula mwili wangu na kunywa damu yangu/ anakaa ndani mwangu na mimi ndani mwake.
5. Kama vile mimi nipo mzima kwa ajili ya baba / Vile pia mwenyi kula mimi atakuwa mzima kwa ajili yangu.
6. Njooni kwangu nyinyi wote munaosumbuka na kubeba mizigo/ mimi nitawatuliza.
7. Chukueni mzigo wangu na mujifunze kwangu/kwani mimi mtu mpole na moyo wangu mnyenyekevu.
8. Mutapata tulizo kwa roho,zenu/ Kwani amri zangu ni lahini, na mzigo wangu ni mwepesi.

## TWINGIE NA FURAHA.

1. Twingie na furaha nyumbani kwa Bwana: E Baba Mungu mkuu.
wote tushangilie tukufu zake kuu: " " " "

2. Tumtuze pia Mwana mkombozi wa watu: E Mwana Mungu mtu.
   Wote tutakasiwe na mateso yake: " " " "
3. Tumpigie aksanti Roho mkarimu: E Roho mtakatifu.
   Aliyetufariji na meema zake kuu:" " "

Daima atukuzwe: 1. Heshima sifa shangwe kwa Baba Mungu mkuu.
" " 2. Shukrani na mapendo kwa Mwana Mungu mtu.
3. Tukufu na furaha kwa Roho mtakatifu

Mungu wa milele utatu mtakatifu daima atukuzwe.

**NJONI WOTE KWAKE** **Zaburi: 94.**

Kiitikio: Baba Mungu twasifu mema ezi yako.

1. Njoni wote kwake Bwana yupo hapa,tuimbe na tusifu mema ezi yake
2. Ni mkubwa kabisa apitaye wote,sifa yake ikuzwe ulimwengu kote.
3. Ni muumba mwongozi wa vyote vilivyo duniani na mbinguni,atukuzwe Mungu.
4. Niye akaumba maji inchi kavu,na tuje tumwabudu tupige magoti.
5. Tuje tumwabudu,kwani muumba wetu,ni Mungu Bwana wetu nasi kondoo zake.
6. Leo tusikie sauti ya Bwana na siye tufungue moyo wetu wote.
7. Sisahau ndugu mababu wo'wetu waliziba sikio,na moyo kwa Bwana.
8. Japo moyo mgumu waliona kweli ajabu na myujiza yake Bwana Mungu.
9. Mungu kachukia mambo yao mengi na hivyo kahukumu wengi wachelewe.
10. Kachelewa hivyo pasipo kuona inchi bora na nzuri,katayarishiwa.
11. Na sasa twaomba utukubalie hapa nyumbani kwako,ili tuingie.
12. Baba Mwana Roho,wote Mungu moja,sifa yenu iweko popote milele.

## TWENDE WOTE BETLEHEMU

Kiitikio: Twende wote Betlehemu kumsalimu Yesu,kazaliwa leo kwetu mtoto wa Maryamu.

1. Saa ya usiku kati kulikuwa kimya na wachunga wa bondeni wamekesha zamu,Mara mbingu ikafunguka na malaika wengi wakashuka wakaimba sifa zake Mungu.
2. Nyi wachunga msiogope na mwande pangoni mutamwona Mwana Mungu ndiyemkombozi.Walikwenda na haraka walivyoambiwa walimkuta Bwana Yesu mtoto mzuri sana.
3. Nasi Yesu tunakuja kukusalimia,tunataka kutolea moyo wetu mzima. Tunakupigia aksanti kwa wokovu wetu,tunataka kwahidia mwendo wetu mzuri.

## TWIMBE ZA YESU.

Kiitikio: Twimbe mshindaji wa Golgotha,Yesu Mwokozi Alleluia.

1. Twimbe za Yesu heshima,amefufuka ni mzima,zambi na kufa kashinda. Kesha mateso na inda.
2. Tusimwogope shetani wala duniani na shani kwa Mwokozi ni mzima. Atatuponya hatima.
3. Yesu twakusadikia japo tabuni twalia kiisha mashaka na giza nasi utatutuliza.
4. Utujalie neemayo tusisahau mer.ayo Yesu katika kiama,mwisho tuache salama.

## E UMUNGU.

Kiitikio: Ewe Yesu Mungu wetu daima,daima,mtakatifu,daima,daima twakusifu.

1. E Umungu nakuabudu mfumbwa chini ya maumbo nami nakunyenyekea kwani sisikii fumbo.

2. Sikuoni sikugusi neno lako naamini,na mwamini Yesu Mungu neno lake ni yakini.
3. Nafahamu kifo chako,ewe Rabi mkate mzima unilishe nikaonje utamuo'tta hatima.
4. E mwokozi kubalie kwa damuo kuniosha,hata kuosha ulimwengu tone moja litatosha.
5. Yesu uliyefumbika nakuomba nijalie nikuone waziwazi kwako daima nitulie.

## EWE MWILI

Kiitikio: Tuabudu tushukuru,kwa mapendo hayo kweli tumependwa mno,kweli tumependwa mno.

1. Ewe mwili wa mwokozi tunakusalimu umeteswa msalabani kwa ajili yetu.
2. Tusalimu pia damu aliyomwagia ndiyo bei ya wokovu na faida bora.
3. Heri sisi bin'Adamu twajaliwa sana,Mungu yuko kati yetu nasi tu salama.

## TUMSIFU YESU KRISTU.

Kiitikio: Tumsifu Yesu Kristu milele Amina.

1. Subuhi napoamka
   Jinalo nitatamka
2. Kengele ikilia
   Kitema ntajibia
3. Kazini naponenda
   Ntaimba nikitenda
4. Chakula napotwaa
   Shukuru za kufaa
5. Ntamsifu mpaka jua
   Jioni likitua
6. Katika kila saa,
   Ntaimba kwa furaha.

## SIFA KWAKO MUNGU BABA YETU.

Kiitikio: Sifa kwa mkate huu na divai,sifa kwa furaha ya kuungana.

1. Sifa kwako,wamchana na usiku;kwa upepo jua na mvua.
2. Sifa Baba,kwa maua ya marangi mazuri;kwa michezo kicheko na furaha.
3. Sifa kwako Baba,kwa wazee na vijana kwa nguvu na maisha uliotupa.
4. Sifa kwa Baba kwa Mwana kwa Roho,leo siku zote.
5. Na ulinde kando njiani mwa mbingu,wandugu zetu waliofariki.

## MALIMWENGU YATAKA KUNIVUTA.

Kiitikio: Sichi kitu,sichi kitu nina Mwokozi nami.

1. Malimwengu yataka kunivuta,ya dunia niwe mtumwa mimi,kunishinda mmeshindwa hamtapata.
2. Ha haya watoto wa dunia kwani nguvu na kuchonga ndimi,mukiungama kwa kunijaribu.
3. Rabi angu mwongoa mambo yote kwako nimetumaini,longeze imani ni sisite.

## EE MUNGU UNIOKOE Zaburi 68.

Kiitikio: Ee Mungu uniokoe,yaani uchungu wanisonga moyo.
1. Nimechoka kwa kulia kwangu,Bwana wangu ee,macho yangu yamekuwa mazaifu,kwa kungoja Mungu wangu.
2. Wanaonichukia bure ni wengi,na nguvu sana,wanataka kunipoteza mbali,wamekuwa hodari,
3. Ee Mungu unajua ujinga,wa roho yangu,makosa yangu yote wazi, mbele ya macho yako.
4. Ninatukanwa kwa ajili yako,ee Mungu wangu,Haya yangu ni kubwa sana,unanifunika uso wangu.

5. Kwa ajili yako nipo mgeni,kwa ndugun zangu,Na mtu asiyejulikana,kwa waana wa mama yangu.
6. Kwani juudi kwa nyumba yako,umenisonga,Na matukano ya wenyi kukutukana,yamemwagika juu ya nafsi yangu.
7. Unajua nini ninasumbua,ee Mungu wangu,Wenyi kunizulumu mengi hivi,wako wote mbele yako.
8. Matukano yanavunja roho yangu,miye maskini,Nimepata haya na matusi,siwezi tena kupona.
9. Nikangoja kwa kunihurumia,wala hakuna,na wakunifariji,wala sikupata mtu.
10. Wakanipa uchungu,chakula changu;nalikuwa na kiu;wakaninywesha siki.

## ENYI MATAIFA PIGENI MIKONO.

Kiitikio: Enyi mataifa pigeni mikono/ Mshangilie Mungu kwa nyimbo za furaha.

1. Kwani Bwana ni wa juu mwenyi kitisho/Mfalme mkuu juu ya dunia yote.
2. Ashusha makabila chini yetu/Na mataifa chini ua miguu yetu.
3. Mungu anapaa katika shangwe/ Bwana kwa sauti ya baragumu.
4. Sifa kwa Baba,Mwana na Roho/ Kama mwanzo na daima na milele Amen.

## GLORIA.

Sifa kwa Mungu jûu;
Na duniani amani kwa watu wenyi mapenzi mema,
Tunakutukuza,tunakubariki,tunakuabudu,tunakusifu we Bwana
Tunakushukuru,Kwa sababu ya sifa yako kubwa: Bwana Mungu,mfalme wambingu Baba Mungu mwenyezi.
Bwana Mungu Mwana wa pekee Yesu Kristu.

Bwana Mungu,Mwana-kondoo wa Mungu,Mwana wa Baba,
We mwondoaji zambi za dunia,tuhurumie,
We mwondoaji zambi za dunia,pokea sala zetu.
We mwenyi kukaa kuume kwa Baba,tuhurumie.
Kwa sababu we peke mtakatifu,we peke yako,Bwana,we peke yako
mkubwa sana,Yesu Kristu.
Pamoja,pamoja na Roho mtakatifu katika sifa ya Mungu Baba Amen.

## GLORIA.

Kiitikio: Sifa,sifa mbinguni sifa,kwa Mungu juu (bis).

1. Sifa kwako Bwana mkombozi wa watu wakosefu.
2. Ubarikiwe Bwana na usifiwe,hapa duniani.
3. Huruma kwako Bwana,pokea nyimbo,na sala zetu.
4. Tunakusifu Yesu tunakuabudu,kwa moyo mwema.
5. Sifa kwako Spiritus Mungu mapendo wa Roho tupu.

## CREDO.

Nasadiki Mungu moja:
Baba Mwenyezi,muumba mbingu na dunia na yoyote yanayoonekana na yasiyoonekana; Na Bwana mmoja Yesu Kristu,Mwana wa pekee wa Mungu. Aliyezaliwa na Baba mbele ya zamani zote,Mungu kwa Mungu mwanga kwa mwanga,Mungu kweli kwa Mungu kweli.
Amezaliwa hakufanyiwa, Ashariki Umungu sawa na baba viumbe vyote vimeumbwa naye.
Aliyeshuka mbinguni kwa ajili yetu sisi watu na kwa wokovu wetu.
Akatwaa mwili kwa tendo la Roho mtakatifu.
Akazaliwa na Bikira Maria,akajifanya mtu,akasulubiwa kwa ajili yetu,wakati wa Ponsyo Pilato,akateswa,akazikwa.
Akafufuka siku ya tatu,kama ilivyoandikwa. Akapanda mbinguni anakokaa kuumeni kwa Baba,atarudi tena na sifa kuamua wazima na wafu. Na ufalme wake papipo mwisho. Na roho mtakatifu Bwana mwenyi kuleta uzima,mwenyi kutoka kwa baba na Mwana,mwenyi

kuabudiwa na kusifiwa,pamoja na baba na mwana;aliyesema kwa vinywa vya manabii na Eklezya moja takatifu Katolika,yenyi asili kwa mitume. Naungama ubatizo moja,kwa maondoleo ya zambi. Nangoja,nangoja,nangoja ufufuo wa wafu,na uzima,na uzima wa milele  Amen,amen,amen.

CREDO

Namsadiki Mungu baba mwenyezi muumba mbingu na inchi
Namsadiki Mungu :Mwanae wa pekee,Bwana wetu Yesu Kristu.
Namsadiki Roho mtakatifu Mungu,mfariji mpaji wa neema:
Tunakusifu we Bwana,twakushukuru mwenyezi;ndiwe Bwana milele, ndiwe Bwana milele.

KYRIE

Bwana,utuhurumie,tunakuchukiza tukikosa mapendo,  Utuhurumie (bis)

Kristu,utuhurumie,tunakuchukiza,tunapokusahau,  Utuhurumie (bis)

Bwana,utuhurumie,tunatupa neema unazotupatia,  Utuhurumie (bis)

WIMBO  WA MATUMAINI.

Kiitikio: Natumaini,natumaini,natumaini,nifike mbele ya Baba.

1. Wajengaji wa neno la Mungu,mujenge na matumaini.
2. Natumaini,kufika kwake,mbinguni kwa baba Mungu.
3. Baba Mungu,alisema;ombeni na mutapewa,tafuteni mutapata.
4. Wandugu zetu,musidanganyiwe,na mambo ya dunia.
5. Wafuatao,na matumaini,watapata tuzo kubwa mbinguni.
6. Ibrahim,kwa imani yake,atumaini vyote alivyoagizwa.
7. Mama Maria,kwa imani yake,alikubali kumzaa mkombozi.
8. Angalia,katika mwanzo,kusura kumi na mbili,utamwona Ibrahim,ni mtu wa imani.
9. Atukuzwe Baba,Na Mwana na Utatu mtakatifu.

## WIMBO WA MATESO.

Kiitikio: Yesu (bis) alikufa msalabani juu yetu,tuwe na mapendo sisi wote wanadamu.

1. Yesu alisema mzaeni matunda mema/Kiisha mutakuwa nyinyi wote wafuasi wangu.
2. Tena wachungaji waliambiwa na Bwana Yesu/Mimi ni mlango wa kondoo za Babangu.
3. Kama vile baba alivyonipenda mimi/ Nami pia nawapenda nyinyi wote.

## :KWA MAJILIO/

Kiitikio: Tengenezeni njia ya Bwana,linganusheeni mapito yake Emmanueli apate kuingia.

1. Mungu mwana amejifanya mtu,mfalme wa Wafalme amejishusha ili akifanana nasi tupewe uzima.
2. Bwana atatujia kutoka Sion na katika kizazi cha Daudi atazaliwa,Bwana anachukua mabegani,kazi na ufalme wa Babake.

## KUSALI NI HERI.

Kiitikio: Ni amri ya Mwokozi/tusali daima kuliko yote kazi/ tufanye hii vema,kuliko yote kazi tufanye hii vema.

1. Kusali ni heri/ni kumtolea Mungu,Baba yetu wa mbingu/heshima hadili.
2. Kusali ni heri/muumba ni kumpenda,neno bora kutenda/na kushika amri.
3. Kusali ni heri/wakati wa uchungu/kukumbuka uwingu/kwa leta Zaburi
4. Kusali ni heri/shetani kumkimbiza/fazila kufuliza/ya sala desturi.
5. Kusali ni heri/kunampa tumaini/na majuto moyoni/mtu aliyekiri.

Archivio Saveriano Roma

6. Kusali ni heri/uwingu wapendezwa/watu wafanyizwa/yafutika shari.
7. Kusali ni heri/ roho inapoitwa/kuona marizawa/ya mbingu fahari.

## KUMSIFU MUNGU

1. Mungu atukuzwe/ Litukuzwe jina lake takatifu.
2. Atukuzwe Yesu Kristu/ Mungu kweli na mtu kweli.
3. Litukuzwe jina la Yesu/Utukuzwem moyo wake mtakatifu.
4. Atukuzwe Yesu/Katika Sakramenta kuu ya altare.
5. Atukuzwe mama mtukufu wa Mungu/Bikira Maria mtakatifu.
6. Atukuzwe Maria mtakatifu/Aliyekingiwa zambi ya asili.
7. Atukuzwe Maria mtakatifu/aliyepalizwa mbinguni.
8. Litukuzwe jina la Maria/Bikira na mama.
9. Atukuzwe Yusufu mtakatifu/mume wake wa usafi bora.
10. Atukuzwe Mungu katika malaika/na watakatifu wake.

## WIMBO WA KUFIKIRI.

Kiitikio: Alleluia,alleluia,alleluia.

1. Msifuni Bwana pahali pake pa takatifu/msifuni katika anga la uwezo wake.
2. Msifuni juu ya matendo yake makubwa/msifuni juu ya ukubwa wake usio na ukadiri.
3. Msifuni na tarumpeta ya sauti kubwa/msifuni na kinanda na kinubi.
4. Msifuni na kigoma na ngoma/msifuni na zeze na kinanda.
5. Msifuni na matoasi yanayolia nguvu/ msifuni na masahani ya shaba yanayo piga shangwe.
6. Sifa kwa Baba,na kwa Mwana na kwa Roho mtakatifu/ Kama ilivyo-kuwa mwanzo na sasa na myaka ya milele.

## WIMBO WA NOELI.

Kiitikio: Mzazi mwema Maria,(bis) ametuzalia Bwana,jina lake
Bwana Yesu.

1. Wachunga wa bondeni,waliona mwanga mkubwa,wakaangaa tetemeka walipoona mwangaza.
2. Wachunga wakasema,walipoksikia wimbo,ukiimbwa kwa furaha.
3. Malaika wakafika,kwa kuwaambia wachunga,twawaleteni habari, mkombozi amezaliwa.
4. Wachunga wakasema,twende nasi kumwabudu.

## NITAKUBARIKIA.

1. Toka katika inchi na jamaa lako..... Nitakubarikia.
2. Nenda katika inchi nitakayokuonyesha....Nitakubarikia.
3. Nitakufanya baba wa taifa kubwa........ Nitakubarikia.
4. Mataifa yote yatapata baraka kwako..... Nitakubarikia.

## E OMBE TATA.

Kiitikio: E Ombe tata,bana bobe bano,(bis) bana bobe bano
basambila muno,mu lubunga lwobe,twasambila tata.

1. Lubunga lwa tata Ombe lwa mwami msoka,tata wetu wa ponga.
2. Twasambila muno mu lubunga lwobe,byose tulinabyo twa uelesha tata.
3. Milinganyo yetu twa uelesha tata,tata wetu wa ponga.
4. Bashu bana bobe,twalila tata,ubuka mu mbuka yobe.
5. Mbuka ya tata Ombe ili misoka,Yatinga mbuka shose.
6. Bana bose ba Ombe,sambishe byose,bya mumabo-o menyu.
7. Sambishishe tata tuye umwesha/Tusambisha u mango.
8. Mango ma tata Ombe,na mwana Ngomu/Ngomu mwami wa ponga.

Archivio Saveriani Roma

9. Mango ma tata Ombe ma natubusha/Tusambishe u mango.
10. Maye wetu Maria wabuta Ngomu/Mwana wobe Ngomu imoyi.
11. Tulinganye umoyimoyi tuye umwesha/u-o uake u mango.
12. Alebulwe tata,na Mwana Ngomu/ Na Mtima musoka.

## NALUMBILA TATA OMBE.

Kiitikio: Nalumbila tata Ombe,sh'utenda lingi,nalumbila tata Ombe.

1. Tata Ombe mwene ponga tata/nitendele bubibwani.
2. Buno bubi bwanisoma tata/ Nitendele bubi bwani.
3. Mulubunga lwobe tata,muli busoka bwingi/ Nitendele tata Ombe.
4. Tata Ombe watendile,wose wanishanga/ta unyata mu mwiyi.
5. Lwenge lwobe tata Ombe,nine nalushanga/Nalumbila tata Ombe.
6. Wibi wani nabule-a,na bulimbya nale-ula/nalumbila tata Ombe.
7. Buno bulimbya na bule'a,na mikyingo na le'ula/nalumbila tata Ombe.
8. Alebulwe tata Ombe,na Mwana wake Ngomu,na Mtima musoka.

## NATUNDA OZO MWILO.

Kiitikio: Natunda ozo mwilo,alleluia (bis).
Mwendile basoga,basoga,Kalaga wanisolela nzila za kubasa mumo,miso mani mamona Yesu.
Mbogombogo za kinsi zikazinda na kinsi nu'kahinga kumona nsoni.

1. Nibi zani nalekula nu busoga nalembela,nukutunda kubasa mwigulu,mwikala basoga.
2. Kalaga wa ponga ningi wibilile nibi zani,nukutunda kubasa mwigulu mwikala basoga.
3. Kino kinsi kikaya nu bilongo bikaya,bwatwelama Kalaga,watutukya mu mibi.

Archivio Saveriano Roma

## MWANA NGOMU TWASHWA UOBE.

Kiitikio: Ii bibyo bayaya,ii bibyo bayaya.

1. Mwana Ngomu twashwa uobe.
2. Tu ueshe mitima yetu.
3. Tu uwile mbogombogo shetu.
4. Tu uloshe usoma uetu.
   Ii bibyo bayaya,ii bibyo bayaya.
5. Tu uloshe mabala metu.
6. "   "   bisetu na binetu.
7. "   "   bana betu.
8. "   "   batu bose.

## TUMBANGYAKULE.

Kiitikio: Tumbangyakule mwana wa Abesha(bis) unga yetu mitima mwana wa Abesha(bis).

1. Abesha tata,abutwa lingi,unga yetu mitima mwana wa Abesha.
2. Malaika watendile (bis) na balangi mukya'anye mwana wenyu abutwa.
3. Twakya'anya mwonya wetu (bis) twakya'anya na busoka na mbogombogo shose.

## WAKATI WA NOELI

Kiitikio: Benyi wabutwa u-o/Mwami wa alamo (bis).

1. Yesu wabutwa u-o/Mwami wa alamo (bis)
   Wabutwa u-o,wabutwa-u-o;Mwami wa alamo.
2. Yesu mwana wa Maria,Mwami wa alamo (bis).
   Mwana wa Maria,mwana wa Maria,Mwami wa alamo.
3. Tuye netu umona;Mwami wa alamo.
   Tuye umona,tuye umona;mwami wa alamo.

Archivio Saveriano Roma

## ONYESHA MUNGU.

Kiitikio: Kwako tunajitolea,ukubali kupokea,mwili wangu,na roho yangu,unilinde vema.

1. Onyesha Mungu uwezo unayetenda kwetu,hekaluni Yeruzalem, vipaji vya wafalme.
2. Uje Roho mtakatifu,fika moyoni mwetu,uzijaze neema ya juu, roho ulizoumba.
3. Wewe uitwaye Mfariji paji la Mungu mkuu,kisima moto mapendo, na mafuta ya roho.
4. Ee we tujulishe Baba,tumujue na Mwana,nawe Roho mtakatifu, tuamini daima.
5. Utukufu Mungu Baba,utukufu na Mwana;pamoja na mufariji,milele na milele.

## WIMBO WA MATOLEO.

### BWANA WETU.

Kiitikio: Bwana wetu,Bwana Mungu mwema na wa uzima,tunakuja kukutolea(bis).

1. Sadaka ya Yesu Mwokozi, Sadaka ya msalaba mtakatifu.
2. " tutolee na Baba " " " "
3. " " kuomba huruma, " " " "
4. " " Mwana kondoo, " " " "

## SANCTUS.

Mtakatifu,Mtakatifu,Mtakatifu,
Bwana wa majeshi...... Hosana.
Mbingu na dunia,...... Hosana.
Tunakuimbia, ...... Hosana.
Wimbo mkuu wa sifa, hosana,hosana juu.

Huyu mbarikiwa, ...... Hosana
Anakuja leo, ...... Hosana
Kwa jina la Bwana ...... Hosana
Tumwimbie leo ...... Hosana,hosana juu.

òòòòòòòòòòòòòòòòòòòòò

## BABA YETU WA MBINGUNI.

Kiitikio: Tuunakusifu ee Bwana pokea sala zetu.

1. Baba yetu wa mbinguni .......Baba
2. Jina lako lisifiwe ....... "
3. Utawalo wako uje ....... "
4. Utakayo yatendeke ....... "
5. Duniani na mbinguni ....... "
6. Tupe leo chakula chetu ...... "
7. Tusamehe makosa yetu ...... "
8. Kama tunasamehe wenzetu ..... "
9. Tuepushe kishawishi ..... "
10. Leo kesho na milele ......"

Archivio Saveriano Roma

## TATA WATUUILILE PONGA. Kirega

Kiitikio: Tata watuuilile ponga,watutumina mwana wobe.

1. Tata watweshishe lwenge/watweshishe lwenge twamanya busoka na bubi.
2. Angi twalola mwikulu/twamona u ponga shobe.
3. Bashu bana bobe,mulya mwa ale/Bashu twali bilubi.
4. Maria,maye wabota /Watubutila Yesu.
5. Maria maye wetu,inyakyi wa Yesu,utusekele netu.
6. Maria nyakyi wa Yesu,inyakyi wa Yesu,alinetu wetu netu.
7. Alebulwe tata Ombe,Mwana Ngomu na mtima muyaya.

## HESHIMA YA WAKRISTU

Kiitikio: Sisi wakristu heshima yetu ni mapendo yake Mungu.

1. Heshima yetu kupendana na wandugu,wewe pamoja nasi,wewe pamoja nasi mpaka kufa.
2. Heshima yetu furaha mbinguni,na watakatifu ,tunamwimbia Mungu, pamoja na malaika mpaka kufa.
3. Heshima yetu,kitumaini kwa Mungu nguvu zetu kwa mateso ya Yesu unatupatia neema,mpaka kufa.

## TULIKUWA NA MWENZETU.

Kiitikio: Tulikuwa na mwenzetu,tulikuwa na mwenzetu
Yule amekwisha kufufuka.

1. Kaburi ni mwanzo, oh oh oh ni mwanzo,kaburi ni mwanzo wa ufalme wa Mungu.
2. Tumaini ni mwanzo " " " " " Tumaini " " "
3. Imani ni mwanzo " " " " " Imani " " "

Archivio Saveriano Roma

4. Mapendo ni mwanzo, oh,oh,oh ni mwanzo mapendo ni mwanzo wa ufalme wa Mungu.
5. Furaha ni mwanzo , " " " " " furaha " " "
6.

Tulikuwa na mwenztu (bis) Yule amekwisha kufufuka.

1. Kiburi ni mwanzo, oh,oh,oh,ni mwanzo kiburi ni mwanzo wa upotevu wa mbingu.
2. Majivuno ni mwanzo oh,oh,oh,ni mwanzo " " " "
3. Fitina ni mwanzo " " " " " fitina " " "
4. Ulozi ni mwanzo " " " " " ulozi " " "
5. Usharati ni mwanzo " " " " " usharati " "
6. Uwongo ni mwanzo " " " " " uwongo " " "
7. Chuki ni mwanzo " " " " " Chuki " " "
8. Uvivu ni mwanzo " " " " " uvivu " " "
9. Uchoyo ni mwanzo " " " " " Uchoyo " " "
10. Na ulevi ni mwanzo " " " " " na ulevi " "

Tulikuwa na mwenzetu (bis) Yule amekwisha kufufuka.

òòòòòòòòòòòòòòòòòòòòòòòò

## ZAMBI ZANGU.

Kiitikio: Zambi zangu tosha baba/we Mungu wa uwema.

1. Tunakupatia nyoyo zetu roho zetu we Mungu wa nguvu tele.
2. Uwe kwa sisi njia ya mbingu,utuhurumie.
3. Uwe kwa sisi katika giza,mwangaza na kiongozi.
4. Tunajua ya kama tupo wakosefu,kweli utuhurumie.

## MUJE MBIO  MBIO.

Kiitikio: Muje mbio mbio kusikia neno la Mungu.

1. Kengele ikilia,tuwe sisi wote nyumbani mwa Mungu.
2. Wababa na wamama,vijana na wabinti.
3. Karibuni wote,walimu wa dini,wafuatao wote.
4. Karibuni pia,wazee wa kanisa,wakristu na walejo.
5. Tumwimbie Mungu,yeye baba yetu,anye na huruma.
6. Tushangilie Rabi,tupige mikono.
7. Tuimbe zaburi,asifiwe Yahwe,kwa kinanda na zeze.
8. Wandugun tutambue,mapendo ni ya lazima,tupende Mungu wetu,pia na ndugu zetu.
9. Wandugu tutambue,amri kumi za Mungu,tatu zataja Mungu,saba zataja watu.
10. Atukuzwe baba na Mwana na roho,utatu takatifu.

òòòòòòòòòòòòòòòòòòòòòòòòòòòòò

## SALA YA KUSADIKI. II

Kiitikio: Namsadiki Mungu baba Mwenyezi,muumba mbingu na dunia.

1. Na vitu vyote vinavyoonekana na visivyoonekana
   Namsadiki Bwana moja Yesu Kristu,Mwana wa pekee wa Mungu.
2. Amezaliwa na Baba toka juu,mbele ya nyakati zote.
   Ndiye Mungu anayetoka kwa Mungu,na mwanga kwa mwanga.
3. Na Mungu kweli kwa Mungu,amezaliwa hakuumbwa/Mwenyi Umungu moja na baba,vyote vimeuumbwa naye.
4. Alishuka toka mbinguni kwake,kwa ajili yetu/na kwa ajili ya sisi watu,na kwa wokovu wetu.
5. Akapata mwili kwa Roho mtakatifu,katika Bikira Maria/
   Akawa mtu akasulubiwa,kwa ajili yetu.

Archivio Saveriano Roma

6. Wakati wa Ponsio Pilato,akateswa akazikwa
akafufuka siku ya tatu,kama ilivyoandikwa.
7. Akapanda mbinguni anapokaa kuume kwa Baba/
Atarudi tena na sifa kuamua/ Wazima na wafu.
8. Na ufalme wake hautakuwa na mwisho,hautakuwa na mwisho/
Namsadiki Mungu Roho mtakatifu,Bwana namleta uzima.
9. Anayetoka kwa Baba na Mwana,anayeabudiwa/
Nakusifiwa na baba na mwana,aliyenena kwa manabii.
10. Namsadiki Eklezya moja,takatifu Katolika/
Iliyotoka kwa mitume,Eklezya Katolika.
11. Naungama Ubatizo moja;kwa maondoleo ya zambi/
Nangoja ufufuo wa wafu,na uzima wa milele.

Sanctus.

Mtakatifu,mtakatifu,mtakatifu (bis)

Upo Mungu mwenyezi mbinguni,upo mfalme mkubwa duniani
wote twausifu ukubwa wako.

Hosana,hosana,hosana, Sifa kwa mwenyi kuja,kwa jina la Mungu
Bwana,Yesu Kristu mfalme,Yesu Kristu mfalme

Hosana,hosana,hosana.

Archivio Saveriani Roma

## TUTUSHIKE OMBE. Kirega.

Kiitikio: Tutushike Ombe, twindilile tata, utukendeleshe, bashu bana bobe.

1. Utushike tata Ombe, tutushike bibene/ Bashu bana bobe tata wa mwikulu.
2. Twa'useka na ponga utulishe netu/ Bashu bana bobe tata wa mwikulu.
3. Tulibose na ngyala, utwi'ushe netu/ Bashu bana bobe tata wa mwikulu.
4. Twabokaboka na piushi yetu/ Bashu bana bobe tata wa mwikulu.

K I M E C H A P W A  P A  M W E N G A
Y U N I  NA  Y U L A I  I 9 7 4.
M W A K A  I K A N D O.

Archivio Saveriano Roma

# Y A L I Y O M O


| | | Pag. |
|---|---|---|
| Jongeeni,wabarikiwa wa Babangu | Zab. 1. | 1. |
| Anasa za dunia zinapeperudhwa | Zab. 2. | 1. |
| Yahwe usimame uniokoe | Zab. 3. | 2 |
| Karibuni enyi mwakosao nguvu | Zab. 4. | 3 |
| Wanaokaa kwako wajaliwa heri | Zab. 5 | 3 |
| Uyapokee vema maombi yangu | Zab. 6 | 4 |
| Ee Yahwe jina lako kubwa sana | Zab. 8 | 4 |
| Kivulini mwake Bwana | Zab. 16 | 5 |
| Bwana yu mchunga wangu | Zab. 22 | 5 |
| Vyote mali ya mwenyezi | Zab. 23 | 6 |
| Karamuni mwa Bwana | Zab. 30 | 7 |
| Abarikiwe Yahwe | Zab. 33 | 7 |
| Mbali ya Bwana nashurulika | Zab. 33 | 8 |
| Kama pongo | Zab. 4I | 8 |
| Uso wako mzuri bora | Zab. 44 | 9 |
| Karibu na Mungu | Zab. 53 | IO |
| Nafsi yangu yakukimbilia daima | Zab. 62 | 11 |
| Tuzisimulie sifa zake Bwana | Zab. 78 | I2 |
| Mwimbeni Bwana | Zab. 97 | I2 |
| Sifa Mungu milele | Zab.102 | 12 |


Archivio Saveriano Roma

Toka chini nakulilia (De Profundis) Zab. 129 13
Shukrani kwa Rabi Zab. 102 14
Nyumbani kwa Bwana Zab. 121 14
Uniokoe Bwana Zab. 108 15
Katika kivuli cha Bwana Zab. 120 16
Bwana asipoijenga nyumba Zab. 126 16
Huruma yake Rabi Zab. L35 17
Rehema za Yahwe Zab. 127 18
Shangwe kwa Bwana Zab. 150 18
Ninapotangatanga,uninyoshee mkono Zab. 12 19
Ukweli wastahili Baraka Zab. 11 19
Utukuzwe Bwana we Zab. 18 20
Vijana wa tatau katika Tanuru(Danieli) 20
Kengele za juu.................................... 2I
Kimya bara ....................................... 2I
Mbali kule ....................................... 22
Lala kitoto cha Mungu ............................ 22
Hodi wachunga .....................................22
Gloria sifa kwake Mungu ...........................23
Ushukie Masiha ................................... 23
Sasa latimia ..................................... 24
Ahadi ya Mungu ................................... 24

Archivio Saveriano Roma

Ave Maria


24

Muumba jua na nyota ........................................ 25
Tukipenda wenzetu ........................................ 25
Huo ndio ni mwanzo ........................................ 26
Aksanti sana Yesu ........................................ 26
Tunapokea Mungu ........................................ 27
Tupo Wakristu ........................................ 27
Shukuruni Mungu ........................................ 28
Kubariki na kugawanya matawi ........................................ 29
Utukufu sifa na heshima ........................................ 29
Tumsifu Yesu ........................................ 29
Tupalize sauti zetu ........................................ 30
Ewe Yesu ........................................ 30
Mama safi sana ........................................ 3I
Yesu kupaa mbinguni ........................................ 3I
Kupaa kwake Rabi ........................................ 32
Tumekuja ........................................ 32
Asiregee moyowe ........................................ 33
Mama pale msalabani ........................................ 33
Binadamu inama kichwa ........................................ 34
Twakuabudu mkate ........................................ 34


Archivio Saveriano Roma

Kikondoo cha Mungu .......... 34
Kumpenda Yesu .......... 35
Alleluia Bwana amefufuka .......... 35
Mbingu inchi na bahari .......... 36
Tuleni wote .......... 36
Tunakuabudu Yesu altareni .......... 36
Nitajongea altare ya Babangu .......... 37
Tunaenda kwa Bwana Yesu.......... 37
Utulishe .......... 38
Kumsifu Mungu .......... 38
Mambo ya ajabu .......... 38
Upokee sala zetu zote .......... 39
Pokea baba matoleo yetu .......... 39
Pokea sisi Bwana .......... 40
Ukubali kuipokea ..........40
Ninakutolea Mungu ..........4I
Pokea Bwana.......... 4I
Baba mwema .......... 42
Twende kwa Mwenyezi .......... 42
Karibu ya Bwana .......... 43
Tumepewa amri ..........43

Archivio Saveriano Roma

Kiapo cha Ubatizo......................................44
Alleluia Bwana amefufuka ..............................44
Ee viumbe karibuni ....................................44
Damu takatifu .........................................45
Mkristu miye ........ .................................45
Hakuna kitu ........................................... 46
Tumsifu Bwana wetu..................................... 46
Tumwimbie muumbaji ....................................47
Tumfuate tumkaribie ...................................47
ALLELUIA............................................... 48
ALLELUIA MSIFUNI BWANA................................. 48
Baba yetu ............................................. 49
Alleluia,alleluia,;;...................................49
Yesu mpole na mnyenyekevu..............................49
Mungu ni mlinzi wa waamini ............................50
Aksanti Bwana;.........................................5I
Nitajongea altare ya Mungu ............................5I
Mama Maria mama .......................................5I
Ave Maria yoo Maria....................................52
Mama Maria mpole ......................................52
E Bikira mwezaji ......................................53
Ee Maria mama mzuri ...................................53
Archivio Saveriano Roma

Bikira wa sifa ( Alma redemtoris Mater) .................. 53
Ave Maria ..........................................54
Litania ya Bikira Maria ............................54
Litania ya Bikira Maria II .......................... 55
Kwa kumsifu Mungu ................................ 57
Onjeni ............................................ 57
Tumsifu Maryamu .................................. 58
Mama Maria jambo.................................. 59
Ee Bwana Yesu ..................................... 60
Mwenyezi amekujaza ................................ 60
Wimbo wa msalaba mtakatifu.......................... 6I
Njia ya msalaba.................................... 6I
Tunakusalimu Bikira Maria............................ 63
Maryamu Bikira,tumshangilie........................ 63
Salamu Malkia wa Mbingu............................ 64
Twakusalimia........................................ 64
We kimbilio letu Zaburi 89 64
Tufike wote kwa misa................................ 66
Kwa Bikira Maria.....................................66
Magnificat...........................................67

Moyo wangu humtukuza Rabi (Magnificat)................ 68
Salam Baba.......................................... 68
Uje Roho muumbaji................................... 69
Njoo wangu mfariji .................................. 69
Umtume Roho yako.................................... 70
Nani yupo........................................... 70
Yesu mwema.......................................... 7I
Ee Yesu mwema kabisa................................ 7I
Pigeni mikononi..... Zab. 46 72
Yahwe amsikilize..... Zab. 19 73
Huzuni yangu ni kali .. Zab. 2I 73
Nanepa kwa uzito wa zambi zangu Zab. 24 74
Furahini ee wanadamu Zab. 32 74
Mungu,wangu,Mungu wangu ............................ 75
Wapandao na machozi Zab.125 75
Mungu ni mchungaji wangu sikosewi kitu ZAB. 22 76
Aksanti Yesu........................................ 76
Yesu mwema.......................................... 77
Tuingie na furaha .................................. 77
Njooni wote kwake..... Zab. 94 78
Twende wote Betlehemu ..............................79
Twimbe za Yesu...................................... 79

Archivio Saveriano Roma

E Umungu ........................ 79
Ewe mwili........................ 80
Tumsifu Yesu Kristu.............. 80
Sifa kwako Mungu baba yetu ...... 8I
Malimwengu yataka kunivuta....... 8I
Ee Mungu uniokoe Zab. 68 8I
Enyi mataifa pigeni mikono.......82
Gloria...........................82
GLORIA 2 ........................83
Credo ...........................83
Credo 2..........................84
Kyrie............................84
Wimbo wa matumaini ..............84
Wimbo wa mateso..................85
Kwa majilio......................85
Kusali ni heri...................85
Kumsifu Mungu....................86
Wimbo wakufikiri ................86
Wimbo wa Noeli (mzazi mwema).....87
Nitakubarikia....................87
Archivio Saveriano Roma

E Ombe tata........................................ 87
Nalumbila tata Ombe................................ 88
Natunda ozo mwilo .................................. 88
Mwana Ngomu twashwa uobe........................ 89
Tumbangyakule........................................ 89
Mwami wa alamo ..................................... 89
Onyesha Mungu....................................... 90
Bwana wetu wetu..................................... 90
Sanctus .............................................. 90
Baba yetu wa mbinguni 2........................... 9I
Tata watu'uilile ponga............................. 92
Heshima ya wakristu................................. 92
Tulikuwa na mwenzetu............................... 92
Zambi zangu...........................................93
Muje mbio mbio...................................... 94
Credo 2 .............................................. 94
Mtakatifu 2.......................................... 95.